# KUCHUNGUZA MAJINA YA WATU MASHUHURI YANAVYOCHANGIA KUIBUA MAJINA YA MITAA KISIWANI PEMBA

**FATMA HAMAD NASSOR**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA KUTIMIZA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.KISWAHILI ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Nathibitisha kwamba aliyetia saini hapo chini ameisoma tasnifu hii inayoitwa Kuchungunguza Majina ya Watu Mashuhuri yanavyochangia kuibua Majina ya Mitaa kisiwani Pemba, na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunukiwa shahada ya Uzamili ya Kiswahili M.A (Isimu) ya Chuo Kikuu cha Huria cha Taznzania.

………………………………………………………

**Dkt. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

…………………...................................

Tarehe

## HAKIMILI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kuzalisha au kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

## TAMKO

Mimi, **Fatma Hamad Nassor**, nathibitisha kuwa kazi hii ni yangu mimi binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyengine yoyote.

…………………….…………………………

Saini

……………………………………………

Tarehe

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa watoto wangu wapendwa Ahmad Ali Salim na Akram Ali Salim pamoja na mdogo wangu mlezi Jamila Hamad Nassor, ili iwe kwao chachu ya kujali na kutafuta elimu kwa bidii.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Menyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kunijaalia uhai, uzima na uwezo wa kufanya utafiti, kuandika mpaka kukamilika kwa kazi hii. Kwa hakika bila ya msaada wa Allah lolote haliwezi kufanyika. Pili napenda niwashukuru wazazi wangu wapendwa mama yangu Zainab Hassan Juma na baba yangu Hamad Nassor Bakari kwa kunizaa, kunilea kwa mapenzi makubwa walionesha juu yangu na kunipa msingi bora wa kutafuta elimu kupitia hali na mali zao. Namuomba Allah awape maisha marefu yaliyojaa kheri na furaha. Tatu nawashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyingine hadi kufikia kukamilika kwa kazi hii. Kwa hakika watu waliotoa mchango wao ni wengi hivyo basi, si rahisi kuwataja wote kwa majina. Ila ninapenda kuwashukuru wote nitakaowataja na niaba ya nisiowataja kwa mchango wao wa kufanikisha kazi hii.

Shukrani zangu zapekee zimwendee msimamizi wa kazi hii Bwana Bakari Kombo Bakari kwa kunishawishi kujiunga katika ngazi hii ya elimu. Naweza kusema kuwa kama si Allah aliyemwezeshayeye kunishawishi ili niweze kujiendeleza kielimu nisingefikia hapa nilipo. Pamoja na hayo pia namshukuru kukubali kuwa msimamizi wangu. Namshukuru kwa moyo wake wa uzalendo, ujasiri na uvumilivu wake mkubwa kwangu tokea hatua ya kuandika pendekezo la utafiti hadi kukamilika kwa kazi hii. Naamini kwamba amenivumilia vya kutosha kwa udhaifu na mapungufu yangu kama binaadamu. Yeye kwangu alikuwa mshauri mwelekezi na mwalimu aliyekuwa hodari na makini pia mweledi katika kazi yake. Wakati wote alinikosoa na kunielekeza kwa busara na hekima ya hali ya juu kila ilipobidi kukoselewa na kuelekezwa. Cha kumlipa sina, ila namuombeya duwa kwa Mwenyezi Mungu ampe

maisha marefu yenye manufaa, amzidishie moyo wa upendo na nguvu aweze kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa na jamii kwa manufaa ya sasa na baadae. Ili wanufaike wengi wa enzi hizi na zijazo.

Aidha ninapenda kuushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya jamii, kwa taaluma, maarifa, ushauri na kwa ushirikiano mzuri walionipa na walioniwezesha kukamilisha kazi hii. Nasema ahsante sana Mungu awape afya njema na awajaalie maisha mema wote hapa duniani na akhera.

Nitakuwa mwizi wa fadhila na shukurani pindi nikiacha kumshukuru mume wangu mpenzi Ali Salim Suleiman, watoto wangu wapendwa pamoja na mdogo wangu mlezi Kwa ustahamilivu wao walionionyesha kwa muda wote niliokuwa katika harakati za kufanya utafiti na kazi hii ngumu ambayo inahangaisha akili na fikra.

Halkadhalika, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu kwa umahiri wao wa kunitia moyo pale ambapo ninakata tamaa ya kuendelea na kazi, kwa kunitia moyo na shauku kwa kunipa msaada wa hali na mali kwa lengo la kufanikisha kazi hii.  Nawashukuru na nawatakia kila la kheri, katika ushindi wenye mafanikio. Pia nawashukuru wafanyakazi wenzangu kwa kunisaidia kwa kunipa muongozo pale ambapo pamenitanza na kuniweka sawa ili kuweza kukamilisha kazi hii. Nawashukuru niliowataja na nisiowataja kwani ni wengi nafasi ni chache siwezi kuwataja nyote. Wote nawambia ahsanteni sana.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza Majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Mtafiti aliongozwa na malengo matatu. Kwanza, kubainisha majina ya mitaaa yanayotokana na majina ya watu mashuhuri kisiwani Pemba, Pili ni kubainisha kazi au dhima zilizowapa umashuhuri watu teuliwa na lengo la tatu lilikuwa ni kueleza sababu zilizopelekea majina hayo kuibuka na kuwa majina ya mitaa. Ili kufikia lengo kuu lililokusudiwa mbinu mbali mbali za utafiti zilihusika. Mbinu hizo ni pamoja na mahojiano na dodoso. Utafiti huu uliongozwa na nadharia jumuishi ambayo iliakisi data za utafiti huu kutokana na maoni yaliyotolewa na watafitiwa na wanajamii kwa ujumla yaliunda data za utafiti huu. Kwa upande wa matokeo ya utafiti, mtafiti aligundua kuwa majina ya watu mashuhuri yanatokana na mambo mbali mbali yakiwemo utawala, kazi ama shughuli wanazofanya wanajamii, haiba ya mtu pamoja na hali ya kipato miongoni mwa wanajamii. Kutokana na sababu hizo mtafiti wa kazi hii amebaini kuwepo kwa mitaa mingi hapa kisiwani Pemba iliyoibuka kutokana na majina ya watu mashuhuri. Kwa ujumla utafiti umethibitisha kwamba ipo mitaa mingi iliyoibuka kutokana na majina ya watu mashuhuri. Amebaini pia umashuhuri wao ulitokana mchanganyiko shughuli mchanganyiko za kijamii. Jambo hilo limefanya mitaa mbalimbali iibuke kutokana na umashuhuri wao.

## YALIYOMO

**UTHIBITISHO**........ ii
**HAKIMILI** ........ iii
**TAMKO** ........ iv
**TABARUKU**........ v
**SHUKURANI** ........ vi
**IKISIRI** ........ viii
**ORODHA YA MAJEDWALI**........ xv
**ORODHA YA VIELELEZO** ........ xvi
**SURA YA KWANZA**........ 1
**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA** ........ 1
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 1.2 Usuli wa Mada ........ 1
1.3 Ufafanuzi wa Mada /Tatizo la Utafiti ........ 2
1.4 Malengo ya Utafiti ........ 4
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti ........ 4
1.4.2 Malengo Mahsusi ........ 4
1.4.3 Maswali ya Utafiti........ 5
1.5 Mawanda ya Utafiti........ 5
1.6 Umuhimu wa Utafiti........ 5
1.7 Vikwazo vya Utafiti ........ 6
**SURA YA PILI**........ 7
**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**....... 7
2.1 Utangulizi ........ 7

2.2 Kuhusu Aina za Majina ... 7

2.3 Kuhusu Majina ya Watu na Asili yake ... 10

2.4 Kiunzi cha Nadharia ... 11

2.5 Ombwe la Utafiti ... 13

2.6 Muhtasari ... 13

**SURA YA TATU** ... 14

**3.0 MBINU ZA UTAFITI** ... 14

3.1 Utangulizi ... 14

3.2 Mkabala wa Utafiti ... 14

3.3 Eneo la Utafiti ... 15

3.4 Sampuli Lengwa ya Watafitiwa ... 16

3.5 Usampulishaji ... 16

3.6 Mbinu za Kukusanyia Data ... 18

3.7 Hojaji (Dodoso) ... 19

3.7.1 Mahojiano ... 21

3.8 Maadili ya Utafiti ... 22

3.9 Mchakato wa Kukusanya na Kuchambua Data ... 22

3.10 Muhtasari ... 23

**SURA YA NNE** ... 24

**4.0 UCHAMBUZI NA UCHANGANUZI WA DATA** ... 24

4.1 Utangulizi ... 24

4.2 Historia ya Kisiwa cha Pemba ... 24

4.3 Majina ya Mitaa yanayotokana na Watu Mashuhuri Kisiwani Pemba ... 26

4.3.1 Jina la Mtaa wa Kwamburi ... 26

4.3.2 Jina la Mtaa wa Chanjamjawiri ........ 27
4.3.3 Jina la Mtaa wa Mkamandume ........ 27
4.3.4 Jina la Mtaa wa Kwakitungu ........ 28
4.3.5 Jina la Mtaa wa Kwamwanamwari ........ 28
4.3.6 Jina la Mtaa wa Kwabomba ........ 29
4.3.7 Jina la Mtaa wa Kisiwani Kwa Bintiabeid ........ 29
4.3.8 Jina la Mtaa wa Kwakiburi ........ 30
4.3.9 Jina la Mtaa wa Kwachambwaga ........ 30
4.3.10 Jina la Mtaa wa Kwamchawi ........ 31
4.3.11 Jina la Mtaa wa Kwasetimende ........ 31
4.3.12 Jina la Mtaa wa Kwakitazonge ........ 31
4.3.13 Jina la Mtaa wa Kiuyu kwa Manda ........ 32
4.3.14 Jina la Mtaa wa Kwashaamemata ........ 32
4.3.15 Jina la Mtaa wa Kwanondo ........ 33
4.3.16 Jina la Mtaa wa Kwasururu ........ 33
4.3.17 Jina la Mtaa wa Kwale ........ 34
4.3.18 Jina la Mtaa wa Kwamatunge ........ 34
4.3.19 Jina la Mtaa wa Ngwachani ........ 35
4.3.20 Jina la Mtaa wa Fiedel Castro ........ 35
4.3.21 Jina la Mtaa wa Ali Khamis Camp ........ 36
4.3.22 Jina la Mtaa wa Pindua ........ 36
4.4 Kubainisha Dhima/Kazi zilizowapa Umashuhuri Watu Teuliwa ........ 37
4.4.1 Umashuhuri na Kazi ya a Mtu aliyeitwa Mburi ........ 37
4.4.2 Umashuhuri na Kazi ya Mtu anayeitwa Mjawiri ........ 38

4.4.3 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Mkamandume .................... 38

4.4.4 Umashuhuri na Kazi ya Mtu alieitwa Kitungu.............................................. 39

4.4.5 Umashuhuri na Kazi ya Mtu alieitwa Mwanamwari..................................... 39

4.4.6 Umashuhuri na Kazi ya Mtu alieitwa Bomba ............................................... 40

4.4.7 Umashuhuri na Kazi ya Mtu anayeitwa Binti Abeid .................................... 40

4.4.8 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Kiburi ................................. 41

4.4.9 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Mchawi ................................ 41

4.4.10 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Chambwaga .......................... 42

4.4.11 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Setimende.............................. 42

4.4.12 Umashuri na Kazi ya Mtu aliekuwa anaitwa Kitazonge ............................... 42

4.4.13 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Manda .............................. 43

4.4.14 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Shaamemata .......................... 44

4.4.15 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Nondo................................... 44

4.4.16 Umashuri na Kazi ya Mtu aneitwa Sururu .................................................... 44

4.4.17 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Mkwale ............................. 45

4.4.18 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyeitwa Matunge .......................................... 45

4.4.19 Umashuri na Kazi ya Mtu aliekuwa anaitwa Ngwachani ............................. 45

4.4.20 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Fiedel Castro...................... 47

4.4.21 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Ali Khamisi....................... 47

4.4.22 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Pindua ............................... 48

4.5 Sababu zilizopelekea Mitaa hiyo Kuitwa kwa Majina ya Watu Teuliwa ...... 48

4.5.1 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwamburi ............................................... 49

4.5.2 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Chanjamjawiri ......................................... 49

4.5.3 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Mkamandume ......................................... 50

4.5.4 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwakitungu ............................................ 51

4.5.5 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Mwanamwari .......................................... 52

4.5.6 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwabomba ............................................. 53

4.5.7 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kisiwani Kwabintiabedi ........................ 54

4.5.8 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwakiburi .............................................. 55

4.5.9 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Chambwaga ............................................ 56

4.5.10 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwamchawi ............................................ 57

4.5.11 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwasetimende ........................................ 57

4.5.12 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwakitazonge ......................................... 58

4.5.13 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kiuyu Kwamanda ................................... 58

4.5.14 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwashaamemata ..................................... 59

4.5.15 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwanondo .............................................. 59

4.5.16 Sababu za Kuibuka kwa Mtaa wa Kwasururu ............................................... 60

4.5.17 Sababu za Kuibuka kwa Mtaa wa Kwale ...................................................... 61

4.5.18 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwamatunge ........................................... 62

4.5.19 Sababu za Kuibuka kwa Mtaa wa Ngwachani .............................................. 62

4.5.20 Sababu ya kuibuka kwa Mtaa wa Fiedel Castro ........................................... 63

4.5.21 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Ali Khamis ............................................. 64

4.5.22 Sababu ya kuibuka Mtaa wa Pindua .............................................................. 65

4.6 Hitimisho ......................................................................................................... 65

**SURA YA TANO** ........................................................................................... 66

**5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ............................ 66

5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 66

5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti ................................................................ 66

5.3 Hitimisho ........................................................................................... 67

5.4 Utoshelevu wa Nadharia iliyotumika ............................................................. 67

5.5 Mapendekezo juu ya Tafiti zijazo ................................................................... 68

**MAREJELEO** .............................................................................................. 69

**VIAMBATISHO** .......................................................................................... 72

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 3.1: Idadi ya Watafiti Waliopewa Kwa Kila Wilaya ............................ 17

Jedwali Na 3.2: Idadi ya Watafitiwa Watakaopewa Dodoso ..................................... 18

## ORODHA YA VIELELEZO

Picha 4. 1: Kutoka Katika Mtandao wa Kimataifa Google ....................................... 25

Picha 4. 2 Picha ya Kuchora Inayoonesha Sura ya Diwani Ngwachani .................. 46

Picha 4. 3: Inayoonesha Chanjaa la Mjawiri Lilivyokuwa Hapo Awali Kabla ya Kuwa Makaazi Ya Watu .......................................................................... 50

Picha 4. 4 Kaburi la Binti Aliyeitwa Mwanamwari ................................................. 53

Picha 4. 5: Makaazi ya Asili ya Diwani Ngwachani ................................................. 63

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

Sura hii ilijikita katika kuangalia taarifa za awali zinazohusu kazi nzima ya utafiti huu. Vipengele vilivyoshughulikiwa katika sura hii ni pamoja na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, mipaka ya utafiti, umuhimu wa utafiti, changamoto za utafiti pamoja na utatuzi wake. Muundo wa utafiti pia umechambuliwa katika surah ii.

### 1.2 1.2 Usuli wa Mada

Majina ni miongoni mwa kategoria ya maneno ambayo imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na Mgullu (1999), Masamba (2004), Khamisi (2010), Kihore na wenzake (2008), Saluhaya (2010) na wengi wengineo. Wote walioshughulikia majina kwa ujumla wao wameeleza kuwa jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, maarifa au tukio katika tungo. Ali na wenzake (1930) wamefafanua kwamba jina ni kila analoitwa binaadamu, mnyama, mmea, vitu vigumu au kitu kingine chochote. Kwa mujibu wa kazi hii mtafiti atalifafanua jina kuwa ni neno linalotaja vitu, watu, hisia, mahali na kadhalika.

Kihore (2004) ametaja aina tatu za majina, ambazo ni majina jumuishi, majina ya pekee na majina ya kikundi. Pia ameeleza kuwa kuna majina ya kawaida kama vile kiti, daftari kalamu n.k. Majina ya pekee ambayo huwa na tabia ya kipekee au mahsusi, majina haya yanaweza kuwa watu, mfano Ali, Fatma, Juma, Majina ya

mahali mfano Uwandani, Mgelema, Kisiwani n.k. Kwa hakika Juma wako wengi duniani lakini kila mmoja yuko tofauti na mwenzake kwa hali tofauti mfano rangi, kimo, tabia, akili na kadhalika. Vivyo hivyo Uwandani ipo Pemba kadhalika Unguja iko Uwandani, lakini yanatofautiana sana kimazingira na asili yake. Majina ya mitaa ni aina moja wapo ya majina ya pekee. Majina haya yanataja miji na mitaa au vijiji. Mfano katika mji wa Chake Chake kuna mitaa mbali mbali kama vile Kwamburi, Chanjamjawiri, Kwasubeti mitaa mingineyo. Kila jina lina sababu zake za kuitwa hivyo. Wataalamu mbalimbali walitafiti majina ya vijiji. Baadhi ya wataalamu hao ni kama Boas (1964) na Schotsman (2003) ambao wameeleza vigezo vya utoaji wa majina ya mahali katika jamii. Buberwa (2010) anaeleza vigezo vya utoaji wa majina ya mahali katika jamii, alitafiti maana zinazoambatana na majina ya mahali. Hivyo majina ya vijiji ni moja wapo ya maneno yanayotumiwa na wanajamii katika jamii zao. Mtafiti wa kazi hii anataka kutafiti kuhusu majina ya watu mashuhuri na jinsi yanavyochangia katika kuibua majina ya mahali (mitaa) kisiwani Pemba.

## 1.3 Ufafanuzi wa Mada /Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza mchango wa majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Watafiti mbali mbali wametafiti kuhusiana na majina ya watu katika jamii tofauti na kubaini mambo mbali mbali yanayochangia au yanavyohusiana na utoaji au upewaji wa majina katika jamii walizotafiti.

Cameroon (1961) anaeleza utoaji wa majina ya mahali katika jamii ya Waingereza. Ametoa aina mbili, kwanza ni yale yanayohusiana na makaazi, kwa mfano Stanford Bridge ni sehemu yenye daraja, Pili ni yale yanayohusiana na sura ya nchi ya eneo

hilo. Hymen (1964) anaeleza majina ya mahali yanayoakisi fikra za watu na pia vipengele vya utamaduni. Omary (1970) alisema kuwa jamii ya Chasu hutoa majina kutokana na vigezo kama muingiliano wa jamii za kigeni, hali ama sura ya nchi pamoja na matukio mbali mbali yanayotokea katika jamii hiyo. Naye Braver (1979:29-30) alibaini mtu mmoja katika jamii ya Wachina hupewa majina tofauti kulingana na nyakati tofauti ambazo anapitia katika maisha yake.

Tafiti nyingi zimebainisha kuwa kuna mambo mengi yanayochangia kuwepo kwa asili ya majina ya mahali, zikiwemo sababu za kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Mlacha (1995) alieleza majina ya mitaa ya Kaskazini Pemba na chanzo chake. Mlacha (keshatajwa) alitoa mfano kwa kusema, Uvuani limetokana na utamaduni wa kuvua. Salim (hajachapishwa) alibainisha majina ya mahali kama vile Ndagoni. Baitan (2010), anasema kuwa, majina ya watu katika jamii ya Wasukuma hutokana na matukio yaliyotokea kipindi cha kuzaliwa mtoto na magonjwa makali yanayompata mtoto wakati akizaliwa. Jamii (2011), alibaini mikabala miwili ya kimaana katika majina ya watu wa kabila la Lulogooli. Mkabala wa kwanza ni mkabala wa maana halisi na mkabala wa pili ni ule wa kimatlaba.

Pia majina ya mahali yametokana na maingiliano ya wageni na wenyeji wa Asia na India. Aliongeza kuwa katika kueleza historia na utamduni wa Waswahili wa mwambao majina kama Malindi, Kiwayu, Pemba na Uziwa yana asili ya Uswahilini. Mlacha (keshatajwa) anaeleza kuwa majina ya mahali ya Waswahili yanaakisi kumbukumbu za yaliyopita yanayohusiana na mambo ya kisiasa au maswali ya kijamii. Katika kuchunguza maumbo ya majina ya mahali katika Kiswahili aligundua

kuna viambishi awali katika baadhi ya majina. Pamoja na wataalamu hao kuchunguza majina ya mahali na asili zake katika jamii mbalimbali, lakini kwa kiwango anachoelewa mtafiti bado tafiti zinazoelezea kwa undani majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitaa au vijiji kisiwani Pemba bado halijafanyiwa kazi. Eneo hili halijashughulikiwa na wataalamu au watafiti waliopita. Hivyo mtafiti ameona ni vyema kulishughulikia eneo hili ili kupunguza mwanya uliopo wa kitaaluma.

Kwa muktadha huu, utafiti huu ulilenga kupunguza mwanya wa kitaalamu ambalo haujitafitiwa kwa kuchunguza mchango wa majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitaa kiswani Pemba.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo ya aina mbili kuu: Lengo kuu na Malengo mahsusi ya utafiti.

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza majina ya watu mashuhuri yalivyo changia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

i) Kubainisha majina ya mitaa yanayotokana na majina ya watu mashuhuri kisiwani

ii) Pemba.

iii) Kubainisha kazi/dhima maalum zilizowapa umashuhuri watu teuliwa.

iv) Kueleza sababu zilizopelekea majina hayo kuibuka na kuwa majina ya mitaa.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo:

i) Ni majina yepi ya mitaa yaliyoibuka kutokana na majina ya watu mashuhuri Kisiwani Pemba?

ii) Ni kazi au dhima zipi zilizowapa umashuhuri watu ambao majina yao yaliibuka kuwa majina ya mitaa Kisiwani Pemba?

iii) Ni sababu zipi zilizopelekea majina hayo kuibuka na kuwa majina ya mitaa?

## 1.5 Mawanda ya Utafiti

Mtafiti alichunguza mchango wa majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Mtafiti kuhusisha na majina ya mitaa ambayo yahusiani na mtu mashuhuri aliepelekea mtaa huo kuitwa jina lake. Utafiti utalifanyika katika kisiwa cha Pemba tu. Kwengineko ambako yapo majina yanayotokana na watu mashuhuri hayakuzingatiwa.

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kutoa mchango mkubwa wa kuongeza uelewa na maarifa kwa wanaisimu kwa kuweza kujua historia ya asili ya mitaa iliotokana na watu mashuhuri kisiwani Pemba na sababu za majina yao kuibuka kuwa majina ya mitaa. Pili, utafiti huu pia utakuwa chachu kwa wataalamu wengine katika kuchunguza zaidi na kuifahamu historia ya miji na mitaa mbalimbali ya kisiwa cha Pemba na kwengineko duniani.

Kazi hii inatarajiwa kuwa kama marejeleo ya kitaaluma yatakayowasidia walimu katika kufundisha na wanafunzi katika kujifunza katika shule za sekondari, vyuo na hata vyuo vikuu.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Katika mchakato mzima wa zoezi la utafiti, mtafiti ailtegemea kukutana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutojibiwa kwa baadhi ya maswali ya dodoso, tatizo la kukosa ushirikiano, suala la rejea zenye kuendana na mada inayotafitiwa.

Mtafiti katika kutatua tatizo la ushirikiano allijitahidi kuwahamasisha na kuwaeleza umuhimu wa kushiriki katika kutoa taarifa sahihi. Kuhusu tatizo la rejea mtafiti alihakikisha kuwa anazunguka na kufanya kila jitihada ili kuhakikisha anapata rejea zinazoendana na mada na pia kuhakikisha anapata rejea zilizo sahihi na zinazoendana na kazi yake. Kuhusu tatizo la kutojibiwa kwa baadhi ya dodoso mtafiti alihakikisha kuwa dodoso zote zinajibiwa kwa usahihi kabisa kwa kuwapa elimu ya kutosha juu ya suala zima la utafiti, hivyo wawe wakweli, wawazi kabisa wakati wa kujaza dodoso hizo. Pale ambapo mbinu ya dodoso haikukidhi haja mtafiti aliteua mbinu mbadala ili kuziba pengo lililoachwa na mbinu ya dodoso.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alipitia maandishi ya wataalamu na watafiti mbalimbali. Mtafiti alisoma kazi ambazo kwa kiasi kikubwa zina ukaribu na mada inayotafitiwa. Pia katika sehemu hii mtafiti aliangalia kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu.

## 2.2 Kuhusu Aina za Majina

Wataalamu mbali mbali wa lugha ya Kiswahili wamejaribu kuandika kuhusu aina tofauti za majina zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa wataalamu hao ni Mgullu (1999) anaeainisha aina sita za nomino au jina ambazo ni Nomino za kawaida, Nomino za dhahania, Nomino za mguso, Nomino zainazohisabika, Nomino za pekee na nomino za jami. Mgullu (1999) anaeleza kuhusu moja ya aina za nomino ambayo ni nomino ya pekee. Nomino za pekee ni nomino ambazo hutaja vitu vya pekee, kitu cha pekee ni kitu mahsusi na ni cha pekee kwa sababu kipo.

Masebo (2006), kwa upande wake ameainisha aina tano za nomino ambazo ni nomino za pekee, nomino za kawaida, nomino za dhahania, nomino za jamii na Nomino za wingi. Anasema hapa duniani, nomino za pekee hutaja majina ya watu, miji, nchi, mito, milima, bahari, maziwa n.k. Kwa muktadha huu majina ya mahali ni moja kati ya majina ya pekee. Vile vile majina hayo hayatolewi tu bali huwa na

sababu mbalimbali zinazopelekea kuzuka kwa majina hayo. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na mila na utamaduni wa jamii husika, au mahali, historia, umashuhuri au umaarufu wa watu.

Kuhusu majina ya mahali Rey (1995) anaeleza kuwa, majina ya mahali ni majina yanayotumika kutambulisha watu au mahali yanayoonesha utofauti baina ya jamii moja na nyengine, kutokana na vigezo vya asili, historia na utamaduni. Hymen (1964) anaeleza kuwa majina ya mahali yanaakisi fikra, watu pamoja na vipengele vya utamaduni.

Massoud (2005) ameelezea asili ya jina la Mtende kuwa ni watu wa Makunduchi Zanzibar ambao walienda kutembea katika kijiji cha jirani wakawakuta wenyeji wa huko wamelima mazao mengi wakasema “ama nyie mtende” wakimaanisha mmefanya kazi kubwa ya kilimo. Nao wakajibu “kwani nyie mjikati Makunduchi”? Na hii ndio sababu ya kupewa jina la Mtende.

BAKIZA (2011) wametaja majina ya mitaa inayopatikana mjini Unguja sehemu alizokuwa akiishi mwanasanaa Jadia mashuhuri Bwana MSA. Wametaja majina ya Kundemba, Baraste Kipande na kadhalika ingawa hawakueleza ni sababu zipi zilizopelekea mitaa hii ikaitwa kwa majina hayo.  Chum (1982) anaeleza asili ya mitaa inayopatikana Mkoa wa Kusini Unguja. Anataja majina kama vile Paje, ambae asili yake ni myama aneitwa Paa pamoja na kilimo cha chooko. Anasimulia kwamba miongoni mwa wageni waliofika Unguja walikuwa ni ndugu saba ambao walishauriana kuishi pembezoni mwa pwani ya Unguja ili waendeleze kilimo cha

chooko. Wakati wakijadiliana, mmoja aliuliza tukiwa na kilimo hiki Paa je? Aliuliza hivyo kwa kuwa paa ni wanyama wanaopenda sana chooko. Kutokana na maelezo hayo mtafiti aligundua kuwa mada ya kuchunguza majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa bado haijafafanuliwa.

Schotsman (2003) anaeleza historia ya maana ya majina ya mahali katika jiji la Dar-es –salam, alitumia majina ya vituo vya daladala na mitaa au kata. Alieleza majina ya vituo vya mabasi yanatokana na majengo kama vile shule, hospitali, kanisa shughuli zinazofanywa na watu katika eneo hilo n.k. Pia majina mengine ya vituo vya daladala hutokana na mwelekeo wa kituo kilipo.

Buberwa (2010) anaelezea majina kutoka katika jamii ya Wahaya akijikita katika majina ya mahali. Buberwa (keshatajwa) anakubaliana kwa kiasi kikubwa na Schotsman (keshatajwa) kwamba majina hutolewa kulingana na shughuli za watu, utamaduni, majanga ya asili n.k. Salim (1984) alieleza asili ya vijiji vya Kusini Pemba kama vile Ziwani na alieleza kwamba mwanzo palikuwa hapaitwi Ziwani bali pakiitwa Mivumo ishirini. Mahali hapo paliitwa hivyo kwa vile palikuwa na mivumo ishirini na baadae pakaitwa Ziwani kwa sababu ya kuwepo ziwa kubwa la maji baridi. Hivyo Ziwani likatokana na hilo ziwa. Kwa kurejelea kazi za wataalamu hawa ambao wameeleza kuhusu majina mbali mbali yakiwemo majina ya jamii ya Wahaya, historia ya majina ya mahali, asili ya mitaa ya Kusini Pemba nakadhalika. Kazi zote hizi zitamsaidia mtafiti katika kuibua mambo mbalimbali yanayohusu mada inayosema kuchunguza majina ya watu mashuhuri na jinsi yalivyochangia kuibu majina ya mitaa kisiwani Pemba.

## 2.3 Kuhusu Majina ya Watu na Asili yake

Wapo wataalamu mbali mbali ambao wameelezea na kufafanua majina ya watu na asili za majina hayo Miongoni mwa watafiti hao ni Chulk (1992), ambae alitafiti kuhusu majina ya watu wa Afrika ambapo anaelezea kuwa kawaida watu hupewa majina kutokana na matukio fulani, vitu vikubwa vya kushangaza, siku au Juma mtu alipozaliwa. Mfano "Aarende" Kiyoruba lina maana ya tuliyekuwa tumemuomba au tumemsubiri. Jina hili limetokana na familia ambayo kwa muda mrefu hawakupata mtoto wa kiume. Utafiti huu umeweza, kumsaidia mtafiti kuweza kujua kuwa kuna maana za majina ambazo zimejificha na maana hizo hujulikana na familia au jamii husika tu.

Kofi (2006), kwa upande wake anaeleza kuwa majina ya Wakaani hubeba ujumbe unaotambulisha muktadha wa kijamii. Dai hili limesimamia hoja ya kwamba majina si yakinasibu bali hutokana na utamaduni wa muktadha wa wazungumzaji wa jamii lugha hiyo. Majina ya watu yanawakilisha namna watu wanavyoishi na kuheshimu mifumo ya tamaduni zao. Utafiti huu ulilenga kuchanganua majina kisemantiki na kugundua vigezo vitumikavyo kutoa majina.

Baitan (2010) alizungumzia majina ya watu katika Kihaya. Katika uchunguzi wake aligundua kuwa majina ya Kihaya yanatokana na matukio fulani, itikadi, jinsi n.k. Mfano Jina la "Ishengoma" hupewa pacha wa kiume aliyetangulia kuzaliwa na Jina la "Nyangoma" huitwa pacha wa kike aliyezaliwa mwanzo. Wanaofuata kuzaliwa wakiwa pacha huitwa" Kato" akiwa mwanamme na "Nyakato" akiwa mwanamke. Manyasa (2010) anaeleza vigezo vtumikavyo kutolea majina ya watu katika jamii ya

Wasukuma. Ameeleza kwamba baadhi ya majina hutokana na matukio yaibukayo kwenye kipindi cha kuzaliwa mtoto. Mfano “Mboku” ni jina la mtoto mwenye uoni hafifu. Mara nyengine jina linaweza kutokana na hadhi ya mtu.

Omary (1970) anaeleza majina ya watu katika jamii ya Chasu na anasema kwamba, majina ya watu yanatokana na vigezo kama mwingiliano wa jamii za kigeni, hali ya kipato, sura ya nchi pamoja na matukio fulani kama vita. Ametoa mifano ya majina kama “Sekona” na “Nankonda” akasema kwamba Nankonda ni mtoto wa kike aliyezaliwa wakati wa vita na Sekona ni mtoto wa kiume aliyezaliwa wakati wa vita. Kwa ujumla tafiti mbali mbali zilizofanywa na zilizosomwa na mtafiti kama ilivyo hapo juu litamsaidia mtafiti kujua Kwamba majina ya watu na pengine hata mahala hayatolewi kiholela, ila huzingatia vigezo maalum vitambuliwavyo na familia husika, au pengine wenyeji wa utamaduni mahususi.

## 2.4 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni mawazo, maelezo, au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2013 414). Massamba (2004) anasema kuwa nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza jambo. Kutokana na maelezo hayo tunaweza kusema kuwa nadharia ni dira na mwongozo wa kukubali jambo kifalsafa, kidini, kimantiki, kijamii na kiutamaduni.

Kwa mujibu wa utafiti huu nadharia ni muongozo ambao mtafiti aliufuata ili kutekeleza uchambuzi wa data zake za utafiti. Utafiti huu ulitumia. Nadharia Jumuishi ya Giles.

Giles (1979) anafafanua kwamba utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamii lugha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii. Hivyo basi majina kama utambulisho wa mtu, kitu, mnyama ni mchakato mmoja wapo ambapo kwamba jamii huyatumia ili kuleta utambulisho. Nadharia Jumuishi ni faafu katika kuchunguza kisayansi majina ya watu mashuhuri na kuibua kwake majina ya mahali kisiwani cha Pemba.

Giles (1979: 253), akiendelea kufafanua kuwa msingi wa nadharia jumuishi unazingatia fasili ya jamii lugha inayosema "jamii inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe". Fasili hii inamulika na kuchota maana halisi ya utambulisho. Hii ina maana kwamba jamii lugha wenyewe inatambua kuwa iko kinyume na jamii lugha nyengine katika masuala muhimu kama vile utamaduni, siasa, uchumi na jamii, kama kiini cha jamii yoyote ulimwenguni.

Elementi hizi za maisha katika jamii ndizo zinazoathiri majina ya watu, ni wazi kuwa ilitumika nadharia ya Giles ili kuweka bayana chimbuko, asili, mazingira na vigezo vitumiwavyo na jamii ya Wapemba kubainisha majina ya watu.
Nadharia ya Giles iliweza kumueleza mtafiti ili aweze kufanya kazi yake ya utafiti kwa kupata majina na mchakato unaoelekeza kupatikana kwa majina yanayopelekea

majina hayo kuitwa majina ya mitaa. Ni uteuzi yakinishi uliotumika kuteuwa nadharia hii (Nadharia Jumuishi) ambayo iliongoza utafiti huu na kuweza kuleta mafaniko. Nadharia Jumuishi ya Giles imeshawahi kufanyiwa kazi na watafiti wengi hapo nyuma na kuleta mafanikio, miongoni mwa hao ni hawa wafuatao:

Masinjila na wenzake walitafiti majina ya watu wa Bara katika kabila la Wachaga na kueleza maana za majina kadhaa yanayojitokeza katika kabila la Wachaga. Mafanikio yaliyopatikana ndio yaliyosukuma mtafiti wa kazi hii kutumia nadharia (Jumuishi) katika kuchunguza majina ya watu maarufu yalivyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba.

## 2.5 Ombwe la Utafiti

Kutokana na kurejelea maandiko mbali mbali sijawahi kuona andiko au chapisho lolote linalogusa majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa. Aidha nimeona ni vyema kulishughulikia eneo hili ili niweze kuziba muachano uliopo wa kitaaluma ambao haujapata kushughulikiwa na wataalamu waliowahi kufanya utafiti kabla ya utafiti huu.

## 2.6 Muhtasari

Sura hii imejaribu kumulika mapitio ya kazi tangulizi, kuhusu dhana ya majina kupitia wataalamu mbali mbali pamoja na kuelezea nadharia muhimu iliyofaa kutumika katika kuandika utafiti huu, sambamba na kutaja ombwe la utafiti ambalo pia limeoneshwa katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili (2004) Mbinu ni njia za kutekeleza jambo. Katika Utafiti mbinu ni njia za kutekeleza utafiti. Katika sura hii tutaangalia mkabala wa utafiti, mchakato wa kukusanya na kuchanganua data pamoja na muhutasari wa mada.

## 3.2 Mkabala wa Utafiti

Walliman (2006) anaeleza mkabala wa utafiti kuwa ni utaratibu ambao mtafiti anauweka wa kukusanya na kuchambua taarifa ili aweze kupata majibu ya maswali aliyojiuliza au kupima mabunio aliyojiwekea kwenye utafiti wake. Utafiti huu utatumia mkabala wa maelezo. Orodho (2009) anabainisha kuwa muundo wa kuelezea tukio ni muundo ambao mara nyingi hutumia njia ya mahojiano na hojaji (dodoso) kukusanya taarifa za utafiti. Ili kufanikisha njia hizi sampuli ya wahojiwa wachache huchaguliwa kwa lengo la kuwawakilisha walio wengi.

Orodho na Kombo (2003) wanabainisha kuwa muundo huu unaweza kutumika kwa tafiti ambazo zina lengo la kujua tabia, mielekeo na mawazo ya watu. Mtafiti atateua muundo huu kwa vile utafiti wake utahusiana na majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa, ulihitaji maelezo kujua maana za majina na vigezo vinavyotumika katika kuwapa watu wa Pemba majina hayo.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza majina ya watu mashuhuri na jinsi yalivyochangia kuibua majina ya mitaa Kisiwani Pemba, sababu zilizopelekea kuitwa majina hayo na shughuli ambazo walikuwa wakijishughulisha nazo watu hao. Utafiti huu ulifanywa katika Kisiwa cha Pemba katika baadhi ya mitaa ya Wete, ChakeChake, Micheweni na Mkoani. Eneo la utafiti lililoteuliwa limekuwa kubwa kwa kuwa majina ya aina hii siyo mengi sana katika eneo lote la Pemba. Isingetosha kuchukua kijieneo kidogo cha utafiti.

Pemba ni Kisiwa kilichoko katika bahari ya Hindi, chenye Mikoa miwili ambayo ni Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Kusini. Kisiwa hiki pia kina Wilaya nne, ambazo ni Wilaya ya Wete, Wilaya ya Chakechake, Wilaya ya Micheweni na Wilaya ya Mkoani.

Wakati wa kukusanya data, data zilikusanywa kama ifuatavyo; Wilaya ya Micheweni, data zilikusanywa katika vijiji vya Wingwi, Micheweni, Kiuyu na Sizini. Wilaya ya Wete, data zilikusanywa katika mitaa ya Wete, Mtambwe, Kisiwani na Wingwi. Wilaya ya Chakechake, data zilikusanywa katika mitaa ya Uwandani, Chanjamjawiri na Pujini pamoja na Gombani.

Wilaya ya Mkoani, data zilikusanywa katika mitaa ya Ngwachani na Mtambile. Mtafiti alichagua Kisiwa cha Pemba kwasababu anayaelewa vizuri maeneo aliyoyafanyia Utafiti huo, kiasi kwamba aliifanya kazi hiyo kwa ufanisi ulio mkubwa zaidi wakati wa kukusanya data.

Katika Kisiwa cha Pemba kuna mitaa mbalimbali ambayo inaitwa kwa majina ya watu ambao ni mashuhuri katika maeneo husika, majina hayo inawezekana yaliitwa kutokana na kazi zao, historia zao au ukoo wao. Kwa upande mwengine, mtafiti alipitia maandiko mbali mbali kupitia maktabani na kwengineko lakini hajaona mtu yoyote aliyefanyia kazi mada inayohusiana na majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitaa Kisiwani Pemba. Kwa maana hiyo mtafiti aliona achague eneo hili katika kufanya Utafiti wake.

## 3.4 Sampuli Lengwa ya Watafitiwa

Keys (1980) anafafanua kuwa sampuli ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa katika kundi kubwa ndio wakilishi wa kundi hilo lote. Sampuli ni istilahi inayotumika kumaanisha watu walioteuliwa kujibu maswalli ya Utafiti kutoka katika kundi husika (Kothari,1990). Sampuli lengwa ni sampuli ambayo mtafiti anakusudia kuitumia katika Utafiti wake (Khamisi; 31).

Sampuli lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huteuwa watafitiwa wake ambao watamsaidia kupata data anazozihitaji ili kujibu masuala yake ya Utafiti (Salim; 27). Sampuli lengwa ya Utafiti huu ni watu waishio katika maeneo mbali mbali katika Kisiwa cha Pemba yakiwemo Wete, Uwandani, Chanjamjawiri, Wingwi na kwengineko.

## 3.5 Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuteua washiriki kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kupata idadi ndogo ya watafitiwa watakaotumiwa katika kutoa data za Utafiti. Usampulishaji ni kitendo cha kuchagua na kupata kikundi fulani ili

kuwakilisha kundi lengwa. Hivyo katika Utafiti huu mtafiti alitumia usampulishaji lengwa. Usampulishaji lengwa ni utaratibu wa mtafiti wa kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha kupata data anazozihitaji mtafiti. Pia ni aina ya usampulishaji ambayo mtafiti huiteua akiwa na imani kwamba, itampatia data itakayomwezesha kufikia malengo ya Utafiti wake. Kwa msingi huu sampuli lengwa ni utaratibu anaouandaa mtafiti ili kupata njia na urahisi wa kupata data anazotarajia kuzipata katika utafiti wake.

Utafiti huu uliwashirikisha watu 76 miongoni mwa hao ni wanawake 38 na wanaume 38. Watu hao walikuwa watu wazima wenye umri wa miaka 40 na 80.
Wakati wa uteuzi wa washiriki mtafiti alizingatia jinsi, jambo ambalo mtafiti ameona kuwa ni muhimu. Lifuatalo ni jedueli linaloonesha kategoria mbali mbali za watafitiwa watakaosampuliwa.

**Jedwali Na 3.1: Idadi ya Watafiti Waliopewa Kwa Kila Wilaya**

| **Jina la Wilaya** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Wete | 10 | 9 | 19 |
| Chake | 9 | 10 | 19 |
| Micheweni | 10 | 9 | 19 |
| Mkoani | 9 | 10 | 19 |
| Jumla kuu | | | 76 |

Chanzo: Data kutoka katika utafi huu

Jaduweli lililopo hapo juu linaonesha kuwa mtafiti aliachagua idadi iliyokaribiana miongoni mwa watafitiwa kutoka kila Wilaya itakuwa na watafitiwa 19 Wakiwemo wanawake na wanaume. Kwa hivyo watafitiwa wote watakikuwa 76.

**Jedwali Na 3.2: Idadi ya Watafitiwa Watakaopewa Dodoso**

| Na. | Jina la Wilaya | Watakaopewa dodoso |
|---|---|---|
| i. | Wete | 9 |
| ii. | Chake | 9 |
| iii. | Mkoani | 9 |
| iv. | Micheweni | 10 |
| Jumla | | 37 |

Chanzo: Data kutoka katika utafi huu

Watafitiwa waliopewa dodoso ni 37, Wilaya tatu waliopewa dodoso ni tisa kutoka kila Wilaya. Wilaya moja waliopewa dodoso ni watu 10 kama inavyoonesha hapo juu. Baada ya dodoso yalifuatia mahojiano na kazi hiyo ilifanywa kama ifuatavyo: -

Idadi ya watafitiwa waliohojiwa

| Na. | Jina la Wilaya | Watakaopewa |
|---|---|---|
| i. | Wete | 10 |
| ii. | Chake | 10 |
| iii. | Mkoani | 10 |
| iv. | Micheweni | 9 |
| JUMLA KUU | | 39 |

Chanzo: Data kutoka katika utafi huu

Jeduweli hili linaonesha kuwa watafitiwa waliohojiwa ni 39 ambapo katika Wilaya tatu kila Wilaya walikuwa na watafitiwa kumi 10 na Wilaya moja kutakuwa na Watafitiwa tisa 9 Hii ni idadi ya watafitiwa wanaume na wanawake.

## 3.6 Mbinu za Kukusanyia Data

Kwa mujibu wa Kothari (2004) mbinu za kukusanyia data ni njia mbali mbali ambazo mtafiti anazitumia ili kupata data anazozihitaji katika utafiti wake.

Adam na Kamuzora (2008) wanasema kuwa data ni vielelezo vinavyokubalika ambavyo vinathibitisha ukweli wa matokeo.

Kwa mujibu wa Pannerselvam (2012) data zimegawika katika makundi mawili , yeye anaona kuwa ziko data za msingi na data za upili.

Pannerselvam anaeleza kwamba data za msingi ni data ambazo hukusanywa na mtafiti uwandani. Data hizi zinaweza kutumika wakati mtafiti atakapofanya utafiti pia watafiti wanaofuatia.

Data za Upili ni data ambazo hukusanywa kutoka kwenye maandishi mbali mbali, kama vile vitabu, ripoti, majarida, machapisho mbali mbali na kadhalika.

Kothari (1990) anafafanua dhana ya ukusanyaji data kama zoezi la awali katika utafiti, ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika malengo yake ya utafiti. Aidha Kothari anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu mtafiti atatumia mbinu ya uwandani ili kuweza kupata data halisi alizozikusudia.

### 3.7 Hojaji (Dodoso)

Mulokozi (1983) anaeleza kuwa hojaji ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti hutayarisha orodha ya masuali au mambo ambayo yanahitajika kujibiwa, kueleza ama kuhojiwa ili kuweza kupata taarifa zinazohitajika katika utafiti.

Enon (1998) anaeleza kuwa hojaji inashabihiana sana na mahojiano. Hii ni kwa sababu njia hii inahusu maswali ambayo yameandikwa ambapo msailiwa anapaswa ayajibu kwa njia ya maandishi.

Woods (2001) anasema kuwa hojaji ni masuali ambayo huhitaji kujibiwa katika mfumo wa maandishi.

Kutokana na maelezo hayo tunaweza kusema kuwa mbinu hii ya hojaji hutumika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa ambapo maswali ya utafiti hupelekwa kwa watafiti wa kwa njia ya maandishi.

Mtafiti alitumia njia hii kutokana na faida nyingi zinazopatikana kwa njia kutumia njia hii.

i) Hojaji ziliweza kupelekwa kwa watafitiwa wengi kwa wakati mmoja.
ii) Maswali yalikuwa sawa kwa watafitiwa wote.
iii) Mbinu hii itarahisisha kukusanya data kwa muda mfupi.
iv) Huwezi kuibua taarifa nyingi kwa katika muda mfupi.

Hojaji ilifanikisha kupata taarifa za majina ya watu mashuhuri alivyochangia kuibua majina ya mtaa. Pamoja na faida hizo kasoro zifuatazo zinaweza kujitokeza;

i) Kutojibiwa kwa baadhi ya maswali.
ii) Watafitiwa wasiojuwa kusoma na kuandika hawatopata fursa ya kujibu maswali hayo.

### 3.7.1 Mahojiano

Mulokozi (1983) anaeleza kwamba mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au simu, kidijitali/barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainsishwa.

Kothari (1990) anadai kuwa mbinu hii inahusu mchakato wa kuuliza maswali ambapo mtafiti anafursa ya kufafanua maswali ambayo hayaeleweki na mtafitiwa / watafitiwa.

Nayo Kamusi ya kiswahili sanifu (2004) inaeleza kwamba mahojiano ni hali ya kuuliza maswali ili kutaka kujua maarifa au uwezo wa mtu juu ya jambo fulani. Ni maswali ambayo mtu huulizwa na mtu au kikundi cha watu pamoja na majibu anayotoa.

Mtafiti aliichagua mbinu hii kwa sababu ina manufaa yafuatayo:

i) Mtafiti alipata fursa ya kufafanua maswali ambayo watafitiwa hawakuyafahamu vizuri.

ii) Mbinu hii ilitoa fursa kwa watafitiwa ambao hawajui kusoma na kuandika kuweza kushiriki katika kutoa taarifa za utafiti.

iii) Mbinu hii ilimpa fursa mtafitiwa kueleza hisia zake binafsi kuhusu mada inayotafitiwa.

iv) Mbinu hii ilitoa fursa ya kuuliza maswali ya ziada na kujibu maswali tokezi yaliyojitokeza katika mahojiano kati ya mtafiti na mtafitiwa.

v) Mbinu hii ilimuwezesha mtafiti kukusanya majina ya mitaa yanayoitwa kwa majina ya watu mashuhuri katika vijij au mitaa yao.

## 3.8 Maadili ya Utafiti

Katika kufanikisha utafiti huu mtafiti ni izo za ukweli. Kwa mujibu wa Sture (20lazima aeleze maadili kwa watafitiwa ili kutoa taarifa bila ya woga na kutoa taarifa zil10) mkabala wa maadili ni moja wapo ya maswala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake.

Pia Adam na wenzake (2008) wanabainisha kuwa maadili ya utafiti ni haki ya kuwa na usiri yaani mtafiti hatatoa siri za mtafitiwa na pia wakafafanua kuwa haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.Kutokana na maelezo hayo mtafiti atahakikisha kwamba kutakuwa na uhuru wa kushiriki katika utafiti huu kwa watafitiwa wote ambao watapata fursa ya kuchaguliwa kushiriki katika utafiti huu.

Kila mtafitiwa atapewa taarifa kamili kuhusu mada ya utafiti ili kuweza kuchangia kwa uwazi zaidi katika kutoa data. Mtafiti atahakikisha kuwa anakwenda sambamba na maadili ya kitaaluma wakati wote wa kutekeleza utafiti wake.

## 3.9 Mchakato wa Kukusanya na Kuchambua Data

Data katika utafiti huu zilikusanywa kwa njia ya hojaji (dodoso) na mahojiano. Mtafiti alitumia mbinu hizi mchanganyiko kwa lengo la kupata matokeo yaliyo bora, kama walivyobainisha Best na Khan (1993) kwamba mbinu moja haijitoshelezi katika kupata data zinazoaminika na kukubalika katika utafiti.

Kwa kiasi kikubwa data katika utafiti huu zitachambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mkabala wa kimaelezo ni mkabala muafaka unaopaswa kutumiwa kufafanua vipengele vya kiisimu kwa sababu isimu huhitaji maelezo ili kufafanua vipengele vyake.

Kothari (keshatajwa) anafafanua kwa kusema kuwa mkabala wa uchambuzi wa data kimaelezo huonesha jinsi watu wanavyofikiri na kuhisi juu ya kitu au jambo fulani. Mkabala huu unafaa kutumika pale mtafiti anapokusanya taarifa kuhusu mawazo ya watu, mitazamo yao, tabia zao pamoja na maswali mbali mbali ya kijamii yanayohitaji maelezo na ufafanuzi. Sambamba na mkabala wakimaelezo mtafiti atatumia njia ya majedwali ili kuziweka data katika hali ya uwazi na kueleweka zaidi. Mtafiti atatumia mkabala wa kimaelezo na jadweli kwa kuzingatia lengo moja baada ya jingine na mwisho ataeleza majumuisho yatakayogunduliwa katika utafiti.
Mkabala huu wa uchambuzi usio wa kitakwimu utachaguliwa na mtafiti kwa sababu utaonekana kuwa ni muafaka kwa utafiti huu kwani lengo la utafiti huu litakuwa ni kuchunguza mchango wa majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa Kisiwani Pemba, ambayo yatahitaji maelezo na sio idadi ambapo pangelihitajika takwimu.

## 3.10 Muhtasari

Sura hii ilizungumzia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, usampulishaji, sampuli lengwa ya watafitiwa ,mbinu mbali mbali za kukusanya data , maadili ya utafiti pamoja na mchakato wa kukusanya na kuchambua data.

# SURA YA NNE

# 4.0 UCHAMBUZI NA UCHANGANUZI WA DATA


## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa kutoka uwandani. Sura hii imejikita katika uchambuzi na kudokeza mambo ya msingi yafuatayo: - Kwanza kabla ya uchambuzi wa data mtafiti ameongelea juu ya historia ya kisiwa cha Pemba. Baadae mtafiti amezungumzia, uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti (1.4.2) na (1.4.3). Uchambuzi wa data za utafiti huu umeongozwa na nadharia jumuishi kama ilivyohainishwa kwenye (2.6). Mkabala wa uchambuzi wa utafiti huu ni wa kimaelezo kwa kiwango kikubwa.

## 4.2 Historia ya Kisiwa cha Pemba

Pemba ni kisiwa kilicho pembezoni mwa mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki; kwenye bahari ya hindi. Kisiwa hiki kina takribani kilomita hamsini (50). Kiko Kaskazini mashariki ya kisiwa cha Unguja na kilomita zipatazo hamsini Mashariki ya pwani ya Tanganyika. Kisiwa hiki kina historia ndefu inayohusiana na kuishi na ukaaji wa binadamu. Wakazi wa kisiwa hiki, kazi zao za asili, ni ukulima, uvuvi na ukwezi wa minazi. Mazao mashuhuri ya chakula yanayozalishwa kisiwani humo ni mpunga, muhogo, maharage, chooko na kunde. Pamoja na haya wakaazi wa kisiwa cha Pemba hujishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara kama vile karafuu, hiliki na pilipili manga. Mji mkuu wa kisiwa cha Pemba ni Chake chake uliojitenga juu ya kilima. Magharibi ya mji wa Chake chake kuna kisiwa mashuhuri kwa maswali ya utalii kiitwacho Misali.

Kimgawanyo Pemba ina mikoa miwili mikubwa ambayo ni mkoa wa Kaskazini na mkoa wa Kusini. Mkoa wa Kaskazini una wilaya mbili; wilaya ya Wete na wilaya ya Micheweni. Mkoa wa Kusini nao pia una wilaya mbili; wilaya ya Mkoani na wilaya ya Chake. Pemba ina majimbo kumi na nane (18) ya uchaguzi kama yalivyotumika katika uchaguzi wa mwaka 2015. Pia Pemba ina shehia 131 ambapo wilaya ya Chake ina shehia 34, Mkoani shehia 36,Wete shehia 36 na Micheweni shehia 25. Kwa asili Wapemba ni watu wenye asili ya uzawa wa kisiwa cha Pemba. Lugha wanayozungumza Wapemba ni lugha ya Kiswahili Cha lahaja ya Kipemba. Pia Pemba ina vijiji ama mitaa mingi mno yenye historia kubwa ya kuibuka kwake. Kila kijiji kina etimolojia yake ya  kupata jina hilo. Ramani inayoonesha kisiwa cha Pemba imewasilishwa hapo chini.




**Picha 4. 1: Kutoka Katika Mtandao wa Kimataifa Google**

## 4.3 Majina ya Mitaa yanayotokana na Watu Mashuhuri Kisiwani Pemba

Kwa kuzingatia malengo mahususi na maswali ya utafiti huu, mtafiti amechambua data za utafiti kwa mnasaba wa lengo mahsusi la kwanza la utafiti lisemalo: Kubainisha majina ya mitaa yatokanayo na majina ya watu mashuhuri kisiwani Pemba. Kwa hakika lengo hilo limekwenda sambamba na swali la msingi la kwanza la utafiti huu lisemalo: Ni majina yepi ya mitaa yaliyoibuka kutokana na majina ya watu mashuhuri kisiwani Pemba? Kwa kutumia mbinu ya mahojiano na dodoso,kutoka uwandani, mtafiti aliibuka na data zinazohusiana na mada yake ambazo ameziwasilisha na kuzichambua kwa kuzingatia lengo na swali hilo la kwanza kama ifuatavyo:-

### 4.3.1 Jina la Mtaa wa Kwamburi

Kwamburi ni mtaa uliopo katika kijiji cha Makaani,wilaya ya Chakechake, mkoa wa kusini Pemba. Mtaa huu kwa upande wa kusini umepakana na machimbo ya kware ya Vitongoji, kaskazini umepakana na makaa ya Uwandani, mashariki umepakana na ukanda wa bahari ya hindi na kwa upande wa magharibi umepakana na ziwa kuu la Kichanje. Kutokana na mahojiano ya vikundi yaliyofanywa kati ya mtafiti na watafitiwa inaonesha kwamba mtaa huu hapo awali ulijulikana kwa jina la Mwisharifu. Kwa sasa hivi mtaa huu umepewa jina la mtu mmoja mashuhuri sana aliyekuwa akiitwa Omari Kheri Vuai (Mburi). Kazi/dhima iliyompa Mburi umashuhuri na sababu za jina lake kuibuka kuwa jina la mtaa zitachambuliwa kwenye lengo la pili na la tatu katika kipengele nambari (4.4.1) na (4.5.1)

### 4.3.2 Jina la Mtaa wa Chanjamjawiri

Chanjamjawiri ni mtaa unaopatikana katika shehia ya Shungi, wilaya ya Chake chake, mkoa wa Kusini Pemba. Kimipaka Chanjamjawiri imepakana na Matale kwa upande wa kusini, kaskazini imepakana na Limani, mashariki imepakana na Pujini na Chanjaani na kwa upande wa magharibi imepakana na Shungi. Wazee wawili; bwana Salim Seif Salim na Salim Mata walipokuwa wanahojiana na mtafiti wa kazi hii walisema mtaa huu hapo mwanzo ulijulikana kwa jina la Kilimani na kwa sasa unajulikana kwa jina la Chanjamjawiri. Mabwana hawa walipoulizwa juu ya kazi ya Mjawiri walisema kwamba, Mjawiri alikuwa ni mtu ambaye hakuwa na kazi maalum, kwa vile bado alikuwa mtoto aliyekuwa chini ya usimamizi wa wazazi wake. Pamoja na ukweli huo Mjawiri alikuwa mashuhuri na pia zipo sababu zilizofanya mtaa huo kuitwa kwa jina la Chanjamjawiri. Sababu hizo zimeelezwa na mabwana hawa pamoja na wahojiwa wengine na zimefafanuliwa kwenye lengo la pili na la tatu katika kipengele (4.4.2) na (4.5.2) vya utafiti huu.

### 4.3.3 Jina la Mtaa wa Mkamandume

Mkamandume ni mtaa unaopatikana katika kijiji cha Pujini, shehia ya dodo, wilaya ya Chakechake, mkoa wa kusini Pemba. Kimipaka Mkamandume imepakana na kijiji cha Mchangani kwa upande wa magharibi. Mashariki imepakana na bahari ya hindi. Kaskazini imepakana na kijiji cha Kijili na kwa upande wa kusini Mkamandume imepakana na Kibaridi. Mtafiti hakupata taarifa juu ya jina la zamani la mtaa huu. Bila shaka yapo mambo yaliyomfanya bwana huyu kupewa jina la Mkamandume. Pia Mkamandume alikuwa na kazi na sababu zilizompa umashuhuri

na zikapelekea jina lake kuibuka kuwa jina la mtaa huo kama itakavyochambuliwa kwenye lengo la pili na la tatu.

#### 4.3.4 Jina la Mtaa wa Kwakitungu

Kwakitungu ni mtaa unaopatikana katika kijiji cha Gombani. Gombani iko ndani ya shehia ya Kwale, wilaya ya Chakechake, mkoa wa kusini Pemba. Awali mtaa wa Kwakitungu ulikuwa ulijulikana kwa jina la Gombani. Sasa hivi mtaa huu unajulikana kwa jina la Kwakitungu. Kwakitungu imepakana na mtaa wa Kwabitimarashi kwa upande wa kusini. Kaskazini Kwakitungu imepakana na Gombani stoo (mabodo). Mashariki imepakana na uwanja mkongwe wa Gombani na magharibi imepakana na mtaa wa Tumbatu. Kitungu ni jina la mtu anayeitwa Bwana Salim Said ambapo kazi na sababu ya mzee huyu kuitwa kwa jina hilo, zitaelezewa na mtafiti hapo baadae ili kukamilisha lengo la pili na la tatu .

#### 4.3.5 Jina la Mtaa wa Kwamwanamwari

Kwa mujibu wa dodoso lililojazwa na watafitiwa Kwamwanamwari ni mtaa uliojulikana hapo awali kwa jina la Kambalu. Kwamwanamwari inapatikana katika shehia ya Wesha, Shehia ya Wesha iko wilaya ya Chakechake, mkoa wa kusini Pemba. kwamwanamwari imepakana na bahari ya hindi kwa upande wa kaskazini. Upande wa kusini imepakana na Wesha, mashariki kunamabonde yanayolimwa mpunga na magharibi imepakana na Kijangwani. Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo juu hapo zamani mtaa huo ulijulikana kwa jina la Kambalu (Mwanamwari). Kazi iliyompa umashuhuri Mwanamwari pamoja na sababu ya mtaa huo kuitwa kwa jina

lake zimechambuliwa kwenye maelezo yanayohusu lengo la pili na la tatu kwenye kipengele (4.4.5) na(4.5.5).

### 4.3.6 Jina la Mtaa wa Kwabomba

Kwabomba ni mtaa unaopatikana katika shehia ya Ole,wilaya ya Chakechake , mkoa wa kusini Pemba. Kwabomba imepakana na Kianga  kwa upande wa kaskazini, kusini imepakana na bonde la mto wa Kwapweza, mashariki imepakana na bonde la mto wa Shanga  na magharibi imepakana na Kanambe (kwa Shekhe Alawi). Mtaa huo hapo awali ulijulikana kwa jina la Mchangani. Kazi iliyompa bwana Bomba umashuuhri na sababu za mtaa huo kupewa jina hilo zimelezwa na kuchambuliwa  na mtafiti kwenye lengo la pili na la tatu la utafiti huu. Uchambuzi huo unaoneka wazi wazi kwenye kipengele (4.4.6) na (4.5.6).

### 4.3.7 Jina la Mtaa wa Kisiwani Kwa Bintiabeid

Kisiwani Kwabintiabeid ni mtaa unaopatikana katika wilaya ya Wete, mkoa wa kaskazini Pemba. Kisiwani Kwabintiabeid ni mtaa uliopakana na Barawa (Kondeawake) kwa upande wa kusini. Kaskazini Kisiwani Kwabintiabeid imepakana na daraja ya Piki. Mashariki imepakana na mto wa Kiuyu (Kilikouchungu) ilhali kwa upande wa magharibi, Kwabintiabeid imepakana na mito ya maji ya chumvi. Ziko dhima ama kazi na sababu kadha wakadha zilizopelekea mtaa huo kuitwa kwa jina la mtu huyo aliyekuwa maarufu sana katika mtaa huo. Ufafanuzi wa madai hayo umeelezwa kwa kina kwenye lengo la pili na lengo la tatu la utafiti huu. Angalia kipengele (4.4.7) na (4.5.7).

### 4.3.8 Jina la Mtaa wa Kwakiburi

Mtaa wa Kwakiburi unapatikana katika maeneo ya Bwagamoyo. Bwagamoyo iko wilaya ya Wete, mkoa wa kaskazini Pemba. Kwakiburi imepakana na Funika kwa upande wa kusini, kaskazini mashariki imepakana na Shengejuu, kaskazini magharibi imepakana na Bwagamoyo. Upande wa mashariki kwa kiburi imepakana na Bahanasa na kwa upande wa magharibi imepakana na Mtambwe. Kiburi ni jina la mtu aliye mashuhuri sana na anaejulikana kwa jina la Ali Rashid Mussa. Hapo awali eneo hilo lilijulikana kwa jina la Bwagu. Kwa hivi sasa mtaa huo unajulikana kwa jina la mtu huyo ambae ni mashuhuri sana. Kazi na sababu ya mtaa huo kuitwa kwa jina la mtu huyo mashuhuri zitachambuliwa na mtafiti katika lengo la pili na la tatu katika utafiti huu. Uchambuzi huu umewekwa wazi kwenye kipengele (4.4.8) na (4.5.8).

### 4.3.9 Jina la Mtaa wa Kwachambwaga

Mtaa wa Kwachambwaga unapatikana katika maeneo ya Wingwi, shehia ya Mgogoni, wilaya ya Wete, mkoa wa kaskazini Pemba. Mtaa wa Kwachambwaga umepakana na Kwazakuani kwa upande wa kusini. Kaskazini umepakana na Kidutani, mashariki umepakana na Mjananza na kwa upande wa magharibi mtaa huo umepakana na Chambwaga jina lake halisi ni Omar Haji. Mtaa huo hapo awali ulijulikana kwa jina la Kwazakuwani. Chambwaga ni jina la mtu ambae ni maarufu sana ambapo alikuwa na kazi zake mbali mbali na pia kuna sababu za mtaa huo anaoishi kuitwa kwa jina lake kama litakavyochambuliwa kwenye lengo la pili na la tatu katika kipengele (4.4.9) na (4.5.9).

#### 4.3.10 Jina la Mtaa wa Kwamchawi

Kwamchawi ni mtaa unaopatikana katika shehia ya Wingwi, jimbo la Pandani, wilaya ya Wete, Mkoa wa kaskazini Pemba. Kimipaka, Kwamchawi imepakana na msitu wa Kidutani kwa upande wa kusini. Kwa upande wa kaskazini mtaa huu umepakana na Kikunguni, ilhali mashariki mtaa umepakana na mava (kwa saha) na kwa upande wa magharibi Kwamchawi imepakana na Makomeni. Jina halisi la mchawi ni Salim Saidi Kassim ambapo kazi ama dhima zake na sababu za mtaa huo kuitwa kwa jina la mtu huyu mashuhuri mtafiti atazieleza katika lengo la pili na la tatu hapo baadae. Angalia (4.4.10) na (4.5.10).

#### 4.3.11 Jina la Mtaa wa Kwasetimende

Mtaa wa Kwasetimende upo katika maeneo ya Wete, shehia ya Kipangani,wilaya ya Wete, mkoa wa kaskazini Pemba. Mtaa huu umepakana na jaa pamoja na soko la samaki kwa upande wa kaskazini, kusini umepakana na Kipanga cha chini, mashariki imepakana na barabara na kwa upande wa magharibi mtaa huo umepakana na Kipangani juu. Setimende ni mtu aliyejulikana kwa jina la Abdalla Setimende ambae alikuwa mashuhuri sana katika mtaa huo. Kazi /dhima pamoja na sababu zilizopelekea mtaa huo zitachmbuliwa kwenye lengo la pili na la tatu katika kipengele (4.4.11) na (4.4.12).

#### 4.3.12 Jina la Mtaa wa Kwakitazonge

Mtaa huu unapatikana katika shehia ya Ole, willaya ya Chake chake, mkoa wa kusini Pemba. Kimipaka mtaa huo umepakana na chuo cha mafunzo kilichoko Kangagani kwa upande wa kaskazini. Kwa upande wa kusini mtaa huu umepakana na Makaa ya

Uwandani, upande wa mashariki umepakana na bahari ya Hindi na kwa upande wa magharibi mtaa huu umepakana na Uwandani na Ole. Katika eneo hilo hapo awali hapakuwa pakiishi watu, hivyo mzee huyo alikuwa ndie mwanzilishi wa mtaa huo. Kitazonge jina lake halisi lilijulikana kama Mussa Omar Mbarouk ambae alikuwa mashuhuri sana. Kazi illiyompa mzee Kitazonge umashuhuri huo na sababu za mtaa huo kuitwa kwa jina lake, zitaelezwa na mtafiti kewnye lengo la pili na la tatu la utafiti huu katika kipengele (4.4.12) na (4.5.12).

### 4.3.13 Jina la Mtaa wa Kiuyu kwa Manda

Kiuyu kwa Manda ni mtaa unaopatikana katika maeneo ya Makangale, wilaya ya Micheweni, mkoa wa kaskazini Pemba. Mtaa wa Kwamanda umepakana na Kifundi kwa upande wa kusini. Kaskazini mtaa huu umepakana na Konde ilhali kwa upande wamashariki umepakana na Msuka .na kwa upande wa magharibi mtaa huo umepakana na Msitu wa ngezi. Manda jina lake halisi ni Jackob Mkamandame Ngema, ambae ni mmakonde kutoka Msumbiji. Bwana huyu alikuwa maarufu sana. Hapo awali mzee Manda aliishi Makangale. Kazi iliyompa umashuhuri mzee huyo na sababu za mtaa huo kuitwa kwa jina la mtu huyo maarufu, zimechambuliwa kwenye lengo la pili na la tatu la utafiti huu, kama ilivyo kwenye kipengele cha (4.4.13) na (4.5.13).

### 4.3.14 Jina la Mtaa wa Kwashaamemata

Huu ni mtaa unaopatikana katika eneo la Micheweni, shehia ya majenzi, wilaya ya Micheweni, mkoa wa kaskazini Pemba. Kwashaamemata imepakana na miembe voti kwa upande wa kaskazini. Kusini imepakana na Mkwaju mgoro, mashariki

imepakana na Chaleni (miembe mingi) na kwa upande wa magharibi mtaa huu umepakana na uzini. Katika eneo hili hapakuwa na mtaa hapo mwanzoni. Mwanzilishi wa mtaa huo alikuwa mzee Shaame. Kazi iliyompa umashuhuri mzee huyo na sababu za mtaa huo kuitwa kwa jina la mtu huyo maarufu, zimechambuliwa na mtafiti katika lengo la pili na la tatu katika utafiti huu kwenye kipengele (4.4.14) na (4.5.15).

### 4.3.15 Jina la Mtaa wa Kwanondo

Huu ni mtaa mpya kabisa ambao umeibuka hivi karibuni. Mtaa huu upo katikati baina ya Micheweni na Kiuyumbuyuni. Mtaa huu unapatikana katika wilaya ya Micheweni, mkoa wa kaskazini Pemba. Kimipaka mtaa huu umepakana na Sheuka kwa upande wa mashariki. Magharibi umepakana na Muombwe, kusini umepakana na Kwansa na kwa upande wa kaskazini mtaa huo umepakana na Kinyuji. Nondo jina lak hasa ni Shehe Juma Juma. Mtaa huu hapo awali ulijulikana kwa jina la Koongoni na kwa sasa hivi unajulikana kwa jina la Kwanondo. Kazi/dhima za mtu huyu zilizompa umashuhuri pamoja na sababu zilizopelekea mtaa huo kuitwa kwa jina hilo zimechambuliwa kwenye lengo la pili na la tatu katika kipengele (4.4.15) na (4.5.15)

### 4.3.16 Jina la Mtaa wa Kwasururu

Kwasururu ni mtaa unaopatikana katika maeneo ya Sizini, shehia ya Sizini, wilaya ya Micheweni, mkoa wa kaskazini Pemba. Mtaa wa Kwasururu umepakana na Mpakani kwa upande wa kaskazini. Kusini mtaa huu umepakana na Ugoni, mashariki imepakana na Kigongoni na kwa upande wa magharibi mtaa huu

umepakana na Mtondooni. Hapo zamani mtaa huo ulijulikana kwa jina la Kigongoni na sasa hivi mtaa huo unajulikana kwa jina la Kwasururu. Sababu zilizomfanya Sururu kuwa mashuhuri na sababu za mtaa wa kigongoni kupewa jina lake zimefafanuliwa kwenye (4.4.16) na (4.5.16).

### 4.3.17 Jina la Mtaa wa Kwale

Kwale ipo katika eneo la Micheweni, shehia ya Kwale, wilaya ya Micheweni, mkoa wakaskazini Pemba. Mtaa huu umepakana na Micheweni kwa upande wa kusini, kaskazini umepakana na Shumba ya mjini, magharibi umepakana na bahari na kwa upande wa mashariki eneo hili limepakana na Micheweni. Kabla ya eneo hili kuitwa kwa jina la mtu huyu maarufu lilijulikana kama msitu wa Micheweni na kwa sasa linajulikana kwa jina la Kwale chupa. Jina halisi la mtu huyu ni Mkwale. Kazi alizojishughulisha nazo pamoja na sababu zilizopelekea mtaa huu kuitwa kwa jina hilo zimechambuliwa kwenye lengo la pili na la tatu katika kipengele (4.4.17) na (4.5.17).

### 4.3.18 Jina la Mtaa wa Kwamatunge

Kwamatunge ni mtaa unaopatikana katika maeneo ya Mkoani wilaya ya Mkoani, mkoani wa kusini Pemba. Mtaa huu umepakana na Tengetenge kwa upande wa kusini, kaskazini umepakana na Mpakani, ilhali kwa upande wa mashariki umepakana na Mtuhaliwa na magharibi mtaa huo umepakana na Mkanyageni. Kabla ya mtaa huo kuitwa kwa Matunge ulijulikana kwa jina la Kichunjuu na kwa sasa mtaa huo unajulikana kwa jina la Kwamatunge. Kazi zilizompa umashuhuri mtu

huyo pamoja na sababu zilizopelekea mtaa huo kuitwa kwa jina hilo zitaelezwa na mtafiti katika kipengele cha (4.4.18) na (4.5.18).

### 4.3.19 Jina la Mtaa wa Ngwachani

Huu ni mtaa uliopo katika shehia ya Ngwachani, wilaya ya mkoani mkoa wa kusini Pemba. Mtaa huu umepakana na Maweni kwa upande wa kusini, kaskazini umepakana na Gongoni. Ama kwa upande wa mashariki mtaa wa Ngwachani umepakana na bonde la kilimo cha mpunga na magharibi umepakana na bonde la kilimo cha mikarafuu . Eneo la mtaa huo hapo awali lilikuwa msitu na kwa sasa mtaa huo unajulikana kwa jina la Ngwachani. Ngwachani alikuwa ni mtawala wa jadi mwenye asili ya Kishirazi. Jambo lililompa umashuri bwana huyu na sababu zilizofanya mtaa huu kuitwa kwa jina lake zimeelezwa na kufafanuliwa kwenye kipengele (4.4.19) na (4.5.19).

### 4.3.20 Jina la Mtaa wa Fiedel Castro

Fiedel Castro ni mtaa unaopatikana katika kijiji cha Vitongoji, shehia ya Wawi, wilaya ya Chake chake, mkoa wa kusini Pemba. Kimipaka Fiedel Castro imepakana na uwanda wa Changaraweni, njia ya kuelekea uwanja wa ndege wa Pemba kwa upande wa kusini. Pia Fidelc Castro imepakana na kijiji cha Jamvini kwa upande wa kaskazini, mashariki Fiedel Castro imepakana na Chuo cha amali, na magharibi imepakana na Kambi ya jeshi. Hapo zamani shule ya Fiedel Castro ilijulikana kwa jina la Said Abdalla Secondary School. Bila shaka Fidel Castro ana mambo yaliyopelekea jina lake kuitwa shule kubwa kabisa na ya mwanzo kwa Pemba pamoja na mtaa kwa ujumla .Pia Fiedel Castro ana kazi na sababu zilizompa

umashuhuri na zikapelekea jina lake kuibuka na kuwa jina la shule na mtaa kwa ujumla kama itakavyochambuliwa kwenye lengo la pili na la tatu, kwenye nukta (4.3.20) na (4.4.20).

### 4.3.21 Jina la Mtaa wa Ali Khamis Camp

Ali Khamis Camp ni mtaa unaopatikana katika maeneo ya Vitongoji, shehia ya Wawi ,jimbo la Wawi, wilaya ya Chake chake, mkoa wa kusini Pemba. Mtaa huu umepakaana na Fiedel Castro kwa upande wa mashariki, kusini umepakana na Furaha, kaskazini umepakana na Vikunguni na magharibi mtaa huu umepakana na Wawi. Zamani mtaa huu ulijulikana kwa jina la kajificheni. Kwa hivi sasa mtaa huu unajulikana kwa jina la Ali Khamisi. Sababu zilizofanya Ali Khamisi kuwa mashuhuri na sababu za mtaa huu kupewa jina lake zimefafanuliwa kwenye (4.4.21) na (4.5.21).

### 4.3.22 Jina la Mtaa wa Pindua

Pindua ni mtaa unaopatikana katika maeneo ya Mkanyageni, wilaya ya Mkoani, mkoa wa kusini Pemba. Kimipaka Pindua imepakana na Bonde la Kihogonikwa upande wa kaskazini, kusini imepakana na kijiji cha Dodea, mashariki mtaa huu umepakana na Barabara ya kuelekea Shidi na magharibi umepakana na bonde la Kwamachungu. Zamani mtaa huu ulijulikana kwa jina la Kibeni. sasa hivi mtaa huo unajulikana kwa jina la Pindua. Sababu za mtaa huo kupewa jina lake zimefafanuliwa kwenye (4.4.22) na (4.5.22).

## 4.4 Kubainisha Dhima/Kazi zilizowapa Umashuhuri Watu Teuliwa

Utafiti huu wenye mada isemayo: Kuchunguza majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Mtafiti kwa kuzingatia mada hiyo ameendeleakuchambua lengo mahsusi la pili la utafiti huu linalosema: Kubainisha kazi/dhima zilizowapa umashuhuri watu teuliwa. Lengo hili limeshabihiana na swali la msingi la pili la utafiti huu linalosema: Ni kazi au dhima zipi zilizowapa umashuhuri watu walioibuwa majina ya mitaa kisiwani Pemba? Baada ya mtafiti kufanya mahojiano na kuwadodosa wakaazi wa mitaa mbali mbali alibaini kuwa watu hao maarufu walikuwa na kazi ama dhima mbali mbali ambazo ziliwapa umaarufu huo kama itakavyoelezwa katika maelezo yafuatayo:

### 4.4.1 Umashuhuri na Kazi ya a Mtu aliyeitwa Mburi

Mburi jina lake halisi alikuwa akiitwa Omar Kheir Vuai. Mzee Kombo Omar Mussaaliyehojiwa na mtafiti tarehe 30/07/2017 alisimulia kwamba “Bwana huyu alipata umashuhuri mkubwa kutokana na kazi ya uganga wa kienyeji aliyokuwa akiifanya. Bwana Mburi alijulikana takriban Pemba nzima na hasa mkoa wa kusini Pemba na vitongoji vyake kutokana na kazi yake hiyo. Mganga huyu aliweza kutibu watu kutoka sehemu mbali mbali za ndani na nje ya Pemba. Alifanikiwa kuwatibu wagonjwa waliokuwa wakisumbuliwa na maradhi tofauti yanayohusiana na tiba za asili. Kituo kikubwa alichokuwa akikitumia kufanyia tiba zake ni nyumbani kwake Mwisharifu. Wakati mwengine bwana huyu alikuwa akiwafuata wagonjwa au wateja wake majumbani mwao kwa lengo la kutoa tiba”. Kwa hiyo kai/dhima iliyompa umashuhuri na umaarufu bwana Mburi ni uganga wa kienyeji wa kutumia mbinu na dawa asilia.

### 4.4.2 Umashuhuri na Kazi ya Mtu anayeitwa Mjawiri

Kwa mujibu wa watafitiwa Salim Seif Salim na Salim Mata ambao walihojiwa tarehe 06/07/2017 wanaeleza kuwa Mjawiri jina lake halisi ni Mjawiri Muhammed bin Abdulrahman.Yeye alikuwa ni mtoto wa Mkamandume (4.4.3) ambae alizaliwa na kukuwa katika mazingira ya kiutajiri. Mjawiri alikuwa muumini mzuri wa dini ya Kiislam, pia alipenda sana kuishi kwa kufuata sheria na misingi ya Kiislam. Mambo yake yote alifanya kwa kumtegemea Mungu pekee. Mbali ya kwamba hakuwa na kazi maalum, lakini alikuwa mashuhuri kutokana na kuwa yeye ni mtu wa nyumba kubwa. Alikuwa ni mtoto wa mfalme; bwana Mkamandume.

### 4.4.3 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Mkamandume

Kwa muijbu wa bwana Salim Seif aliyehojiwa na mtafiti tarehe 21/07/2017Jina halisi la mtu huyu lilikuwa ni Muhammed bin Abdulrahman. Bwana huyu alikuwa ni mtawala katika eneo la Pujini. Na kwa hakika aliweza kuwatawala wakaazi wa Pujini. Kama ilivyo kawaida ya mtawala wa kikoloni, hakuacha kuendeleza madhila dhidi ya wakaazi hao. Aliwatesa na kuwanyanyasa kupitia njia tofauti kama vile kuwatumikisha mashambani, kuwang'oleshaa na kuwabebeshaa mawe kwa ajili ya kujenga kasri lake. Inasemekana mawe hayo walilazimika kwenda nayo katika maeneo waliyotakiwa kuyapeleka huku wakiwa wanasota na kutambaa. Alifika kuwahasi wanaume kwa kuwavunjia nguvu zao za kiume. Jambo hili inasadikiwa ndilo lililomfanya aitwe Mkamandume. Aliwalazimisha wakaazi wa Pujini kubanja chikichi kwa kutumia meno yao.

### 4.4.4 Umashuhuri na Kazi ya Mtu alieitwa Kitungu

Kitungu ni mzee ambae alikuwa anaishi katika maeneo ya Gombani kongwe. Bwana huyu alikuwa ni mtu maarufu sana kwa kazi ya kupiga ramli. Watafitiwa waliofanya mahojiano na mtafiti mnamo tarehe 9/7/2017 walifafanua kuwa, Kitungu alijulikana kwa jina la Salim Said. ambae alikuwa mpiga ramli mashuhuri katika mji wa Chakechake na takriban mkoa mzima wa kusini Pemba. Bwana huyo aliweza kuagua mambo mbalimbali yaliyowasumbua watu wengi yakiwemo mambo ya kindoa na biashara na aliwaelekeza jinsi ya kuyatatua matatizo yao na watu wengi walifanikiwa kwa kiasi kuondokana na matatizo hayo yaliyowasumbua kwa muda mfupi ama mrefu.

### 4.4.5 Umashuhuri na Kazi ya Mtu alieitwa Mwanamwari

Kwa kurejelea kwenye kipengele (4.3.5) kama alivyoeleza mtafiti, watafitiwa mbali mbali waliohojiwa tarehe 9 Julai 2017 walieleza kuwa Mwanamwari jina lake halisi halikuwahi kujulikana. Waliendelea kueleza kwamba, Mwanamwari alikuwa mtoto wa Afandi Mwene. Mtoto huyu alizaliwa na kukulia katika mazingira ya kifalme na utajiri. Mwanamwari alikuwa muumini mzuri wa dini ya kiislamu. Pia alikuwa akipenda kuishi kwa kutekeleza sheria na maamrisho ya Kiislamu. Kijana huyu aliweza kuiunganisha familia yake na watu mbali mbali ambao hawakuwa katika familia moja. Umashuhuri wake ulikuwa mkubwa kwa sababu tatu. Kwanza alikuwa binti wa ukoo wa tabaka la juu. Pili alikuwa muunini wa dini ya Kiislamu aliyewazidi wengi kiutekelezaji. Tatu upeo wake kisosholojia ulikuwa ni wa kupigiwa mfano.

### 4.4.6 Umashuhuri na Kazi ya Mtu alieitwa Bomba

Kama tulivyokwisha eleza hapo awali katika kipengele (4.3.6) ya kwamba kuna watafitiwa waliofanyiwa mahojiano na mtafiti. Miongoni mwa watafitiwa waliohojiwa ni Maimuna Said Rashid na Fadia Saleh Juma. Mahojiano kati yao na mtafiti yalifanyika siku ya tarehe 13 – 7 – 2017. Katika hoja zao walielez kwamba, bwana Bomba ni mzee ambae alikuwa mkulima wa mazao mbali mbali yanayolimwa katika maeneo ya Makaani. Aliweza kulima mazao ya chakula pamoja na biashara. Kazi yake hiyo ya ukulima iliweza kumuendeleza vizuri, na kuyafanya maisha yake kuwa bora. Bwana Bomba alikuwa akipenda kusema kwa sauti kubwa sana, kiasi kwamba sauti yake iliwakera baadhi ya watu waliomsikia wakati akizungumza. Jambo hili lilimpatia umashuhuri mkubwa mtu huyu na likapelekea kujulikana katika maeneo ya Ole pamoja na vijiji vya jirani, vya Uwandani, Mzingeni, Gawana na vyenginevyo.

### 4.4.7 Umashuhuri na Kazi ya Mtu anayeitwa Binti Abeid

Kama mtafiti alivyobainisha kwenye kipengele (4.3.7) Bintiabeid ni mwanamke ambae alijishughulisha sana na kazi ya biashara. Binti huyo aliweza kuchukua bidhaa mbali mbali kutoka Oman na kuleta Pemba kwenye maeneo ya Kisiwani na Vitongoji vyake. Watu walioishi katika maeneo hayo waliweza kufaidika na biashara hizo kwa vile wenyeji hao hawakua na bidhaa kama hizo. Kwa hakika waliweza kubadilishana bidhaa hizo kama ambavyo walikubaliana. Pia aliweza kujinunulia mashamba mengi sana na makubwa ya mikarafuu hivyo takriban asilimia 70 ya mashamba yalioko Kisiwani yalikua ya kwake. Kazi hii ilimpa umaarufu mkubwa sana binti huyu hadi kufikia Kisiwani kuitwa kwa jina lake.

### 4.4.8 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Kiburi

Kwa kurejelea kwenye kipengele (4.3.8) Kiburi aliejulikana kama Ali Rashid Mussa ambae ni mfanyabiashara mashuhuri wa mazao ya biashara hasa karafuu. Bwana huyu ni mtu tajiri kwa vile anamiliki mashamba makubwa makubwa ya mikarafuu ukilinganisha na wenye mashamba wengi walioko katika maeneo ya Bwagamoyo na Mtambwe kwa ujumla. Bwana Kiburi ameandaa mtaa ambao ni mpya kwa kujenga nyumba zake za kuishi, hospitali, nasari, bekari na majengo mengineyo. Kazi hii imempa umashuhuri mkubwa sana hasa kwa vile ni tajiri katika eneo hilo. Kwa kweli biashara zake za karafuu zimemng'arisha na kumpa umashuhuri mkubwa.

### 4.4.9 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Mchawi

Mchawi ni mfanyabiashara mkubwa wa vitu kama nguo za watu wa rika zote pamoja na vyombo vya matumizi ya nyumbani kama vile sahani, sinia, ndoo, vikombe, mabakuli, na kadhalika. Pamoja na hayo Mchawi ni mtu anaependa mashirikiano sana na watu wengi katika jamii yao. Bwana huyo ni mtu aliyeaminiwa na watu wengi kutokana na tabia yake ya ucheshi kwa watu na kupenda kutenda mambo mema jambo ambalo hata dua zake anazoziomba kwa mola wake mara nyingi ni zenye kukubaliwa. Hivyo watu wamejenga imani kuwa mzee Mchawi akikuombea dua au akikwambia jambo kuwa litafanyika basi litafanyika kama alivyosema yeye. Kwa kuwa watu walijenga imani hiyo bwana Mchawi alizidi kupata umaarufu mkubwa katika wilaya nzima ya Micheweni na baadhi ya maeneo mengine yaliyozunguka nje ya wilaya hiyo.

### 4.4.10 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Chambwaga

Kwa mujibu wa watafitiwa waliohojiwa tarehe 15 – 7 – 2017 wanaeleza kuwa Mzee Chambwaga ni mvuvi, mpigaji na mchezaji wa ngoma ya boso, pia ni mfanyabiashara. Chambwaga pia alikuwa muuza duka wa vitu vidogo vidogo kama vile tumbaku, sukari, chumvi na kadhalika. Watafitiwa walizidi kueleza kuwa Bwana huyu aliweza kupiga ngoma ya boso wakati wowote pindi tu akijisikia kujifurahisha mwenyewe katika sherehe mbali mbali kama vile harusi, ushindi wa vitu fulani na kadhalika. Hivyo kazi zote hizi alizokuwanazo bwana Chambwaga zilimpa umaarufu mkubwa sana katika maeneo ya Wingwi na vitongoji vyake.

### 4.4.11 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Setimende

Setimende ni mtu alieishi maeneo ya Kipangani Wete. Bwana huyu alikuwa ni tajiri wa Kihindi aliejishughulisha na kazi ya ufundi wa vyombo vya moto kama vile magari, pikipiki, vespa na kadhalika. Aliweza kutengeneza vyombo hivyo kutoka maeneo mbali mbali ya mji wa Wete na maeneo ya jirani. Kutokana na kazi yake hiyo Bwana Setimende aliweka kituo kikuu cha kutengeneza vyombo hivyo nyumbani kwake. Kituo hicho kiliitwa Gereji ya Setimende. Hivyo kutokana na kazi yake hiyo, Setimende alikuwa maarufu sana katika mji wa Wete na vitongoji vyake vyote jambo ambalo lilipelekea mtaa huo kuitwa kwa jina lake hadi leo hii.

### 4.4.12 Umashuri na Kazi ya Mtu aliekuwa anaitwa Kitazonge

Kwa mujibu wa watafitiwa waliododoswa mnamo tarehe 17 Julai 2017 ambapo miongoni mwao ni Mussa Omar Mussa na Fatma Shaali Ali walieleza kuwa Kitazonge alikuwa mkulima na mganga wa kienyeji. Bwana Kitazonge

alijishughulisha na kilimo kama vile njugu nyasa, tungule na mpunga, pia aliweza kutibu watu wengi kutokana na maradhi yaliyowasumbua. Ingawa alijitahidi kutibu watu mbali mbali na baadhi yao alifanikiwa na wakati mwengine hakufanikiwa hivyo aliweza kuvurumisha tu tiba hizo. Kutokana na kuwa na kazi hiyo ya uganga ilimuwezesha Bwana huyo kuwa maarufu sana katika maeneo yake aliyoishi.

### 4.4.13 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Manda

Tukirejelea katika kipengele (4.3.13) Manda ni mtu aliejulikana kwa jina la Jackob Mkamandame Ngema. Bwana huyu alijishughulisha na kazi ya kilimo pamoja na ufugaji. Watafitiwa waliododoswa na kuhojiwa siku ya Jumatano tarehe 20/8/2017 walieleza kuwa Mzee Manda alikuwa Mmakonde aliyependa sana kulima mpunga na muhogo. Pia bawana huyu alipenda kufuga mifugo mbali mbali kama vile ngombe, mbuzi, punda, kuku na bata. Wakaazi wengi wa maeneo hayo hawakuwa wakijishughulisha na ufugaji wa aina hiyo. Pia mzee huyo alikuwa muumini mkubwa wa dini ya kikristo ingawaje wakati huo hakukua na makanisa katika maeneo aliyoishi. Watafitiwa walizidi kueleza kuwa wamakonde wengi walioishi Pemba walikuwa na itikadi ya kuwa mtu akiumwa sana wanamchinja na kuila nyama yake hivyo imani hii ilitawala sana katika ubongo wa mzee Manda. Mara moja aliumwa sana na kwa hivyo kutokana na khofu ya kuchinjwa na wamakonde wenziwe, ilimlazimu mzee huyu kuhama eneo alilokuwa akiishi awali na kuhamia Kiuyu. Kutokana na kazi hiyo Manda alikuwa maarufu sana katika maeneo hayo ya kiuyu na Makangale kwa ujumla.

### 4.4.14 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Shaamemata

Kwa mujibu wa watafitiwa waliohojiwa tarehe 21/7/2017 wakiwemo mzee Dawa Juma na ndugu Asha Mohammed Makasi wamefafanua kuwa bwana Shaame alijishughulisha na kazi ya uvuvi, kilimo pamoja na masuala ya kisiasa. Kazi ya uvuvi ilimsaidia sana katika kujipunguzia ukali wa maisha. Siasa nayo ilimsaidia katika kujijenga kijamii. Watafitiwa walieleza kuwa eneo aliloishi mzee Shaame lilitumika kama ni sehemu ya kufanyia mikutano ya kisiasa ingawa alikuwa akiishi yeye na familia yake tu. Kazi hizi ndizo zilizompa umaarufu mkubwa bwana Shaame katika maeneo mbali mbali ya Micheweni pamoja na vitongoji vyake.

### 4.4.15 Umashuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa anaitwa Nondo

Tukirejelea katika kipengele (4.3.15) Nondo ni kijana tajiri ambae ni maarufu katika maeneo ya Micheweni. Kijana huyu anaishi baina ya Micheweni na Kiuyum-buyuni. Kijana huyu kwa hakika anajishughulisha na biashara za aina mbali mbali hasa biashara ya magari ya kubeba abiria na mizigo. Magari hayo ambayo yameenea katika kila kona ya wilaya ya Micheweni yameweza kumpatia umaarufu mkubwa bwana Nondo.  Kutokana na kazi hiyo kijana Nondo amekuwa maarufu katika wilaya ya Micheweni na maeneo mbali mbali ya Pemba kwa ujumla.

### 4.4.16 Umashuri na Kazi ya Mtu aneitwa Sururu

Kama mtafiti alivyobainisha kwenye kipenele (4.3.16) Sururu ni mzee ambaeanajishughulisha sana na kazi ya biashara kama vile kumiliki magari, kituo cha afya, kituo cha kutwanga na kusaga mipunga, mahindi na kadhalika. Watu wanaoishi jirani na mzee huyo na wanaoishi maeneo mbali mbali wamefaidika na

huduma hizo. Hivyo kazi hiyo imempatia umashuhuri mkubwa sana Bwana Salim Sururu katika kila kona ya wilaya ya Micheweni.

### 4.4.17 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Mkwale

Kwa kurejelea kipengele (4.3.17) Mkwale alikuwa mkulima na mvuvi alijishughulisha na kilimo cha Mtama, Uwele, muhogo na migomba. Watafitiwa walipohojiwa na mtafiti walieleza kuwa bwana Mkwale alikuwa akijitafutia riziki zake kupitia kazi hizo. Hivyo kutokana na kuwa na kazi hiyo bwana huyo alipata umaarufu mkubwa katika maeneo anayoishi.


### 4.4.18 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyeitwa Matunge

Matunge Jina lake halisi ni Khadija Salum. Kazi ya bibi huyu ni kutibu maradhi mbali mbali yanayowasumbua watoto na watu wazima kupitia dawa za asili. Watu kutoka maeneo mbali mbali ya Pemba hufika nyumbani kwake kwa ajili ya kutafuta tiba ya maradhi na matatizo yanayowasumbua. Kazi hii imempatia umaarufu mkubwa Bi Khadija katika maeneo ya Mkoani. Amenasibishwa na mganga mashuhuri aliyekuja hapa visiwani kutoka Tanzania bara, mnamo mapema miaka ya 200. Mganga huyu alikuwa akiitwa matunge na bi Khadija nae akaitwa Matunge.

### 4.4.19 Umashuri na Kazi ya Mtu aliekuwa anaitwa Ngwachani

Kwa kurejelea katika kipengele (4.3.19), watafitiwa walieleza kuwa Jina halisi la mtu huyu ni Ngwachani. Bwana huyu alikuwa mtawala miongoni mwa watawala wa Jadi wa Pemba. Kama inavyoeleweka kuwa visiwa vya Zanazibar vilikuwa na tawala

za kijadi. Kiongozi wa jadi wa Unguja aliitwa Seheha na kiongozi wa jadi Pemba aliitwa Diwani. Hivyo Ngwachani alikuwa Diwani wa pili na wa mwisho aliyetawala Maeneo ya Pemba hasa Mkoani katika mtaa wa Ngwachani.  Jambo hili kwa hakika lilimpa umashuhuri mkubwa. Picha iliyopo chini ni ya kuchora. Picha hii  inaonesha muonekano halisi wa sura ya diwani Ngwachani ilivyokuwa.



**Picha 4. 2 Picha ya Kuchora Inayoonesha Sura ya Diwani Ngwachani**

#### 4.4.20 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Fiedel Castro

Kwa mujibu wa bwana Khamis Rashid Nassor aliyehojiwa na mtafiti tarehe 30/9/2017 Fiedel Castro ndilo jina halisi la bwana huyo. Mtu huyu alikuwa Raisi wa Cuba katika bara la Amerika ya kusini. Kwa hakika Raisi huyo aliweza kutoa mchango mkubwa sana katika kulikomboa bara la Afrika ikiwemo nchi ya Tanzania. Alitoa misaada mbali mbali ya mafunzo ya kijeshi. Fidel Castro aliwaelimisha Watanzania juu ya umuhimu wa uhuru na kujitegemea. Bwana huyu aliungwa mkono na wanafalsafa mbali mbali akiwemo Mwalimu Nyerere katika falsafa yake ya ujamaa na kujitegemea. Alitoa misaada mbalimbali katika elimu ikiwemo kuijenga shule ya Said Abdalla Secondary School. Msaada huo wa kitaaluma aliotoa Raisi Fiedel Castro ulijumuisha ukarabati wa majengo pamoja na ujazaji wa samani katika shule hiyo. Kutokana na msaada wake huo shule ya Saidi Abdalla ikabadilishwa jina la asili na kupewa jina la Fiedel Castro. Jina hilo lilianza kutumika kama jina la shule na baadae mtaa mzima ukaitwa kwa jina la Fiedel Castro.

#### 4.4.21 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Ali Khamisi

Kwa kurejelea kwenye kipengele (4.3.21), Ali Khamis David a alikuwa injinia wa jeshi la wananchi la Tanzania (JWT). Alikuwa ni mtaalamu katika fani ya ukarabati wa magari ya kijeshi na magari ya watu binafsi. Pia alikuwa miongoni mwa wanamapinduzi ambae alioshiriki katika kuipindua utawala wa kikoloni uliokuwepo hapa Zanzibar. Kazi hii iilmpa umashuhuri mkubwa bwana huyu na kumng’arisha ndani na nje ya jeshi la wananchi. Kwa kuwa alikuwa injinia wa mwanzo kuwepo katika kambi hiyo pia alikuwa mwanamapinduzi mkongwe. Kwa sababu hizo mbili

kambi hiyo ikaitwa kwa jina lake jambo ambalo lilipelekea mtaa wote kuitwa kwa jina la Ali Khamis Camp.

### 4.4.22 Umashuhuri na Kazi ya Mtu aliyekuwa akiitwa Pindua

Kwa mujibu wa watafitiwa waliohojiwa na kudodoswa tarehe 2/10/ 2017 akiwemo bwana Salim Mohd Vuaa wote kwa pamoja walieleza kuwa jina halisi la mtu huyo ni Mohd Juma Pindua. Bwana huyu alikuwa mkulima na mwana siasa mkongwe katika maeneo ya Mkoani na vitongoji vyake. Pia bwana Pindua alikuwa mwanamapinduzi mkubwa ambae alisaidia sana katika harakati za kuikomboa Zanzibar. Bwana huyu alitumia muda wake wote kwa kushirikiana na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi ili kuleta maendeleo hapa Zanzibar. Kutokana na jitihada zake hizo baada ya kujengwa shule mpya katika eneo la Mkanyageni, Raisi wa Zanzibar na mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi aliamua shule hiyo kuipa jina la Mwanamapinduzi huyo ili kuendelea kumuenzi na kuthamini juhudi zake katika kuleta maendeleo. Jina hilo lilizoeleka na kupelekea mtaa mzima kuitwa kwa jina la bwana huyo badala ya shule pekee.

## 4.5 Sababu zilizopelekea Mitaa hiyo Kuitwa kwa Majina ya Watu Teuliwa

Mtafiti ameendelea kuzingatia malengo na maswali ya utafiti ipasavyo kwa kurejelea lengo la tatu la utafiti huu lisemalo: Kueleza sababu zilizopelekea majina hayo kuibuka na kuwa majina ya mitaa. Ni dhati kwamba lengo hilo limekwenda sambamba na swali la msingi la tatu linalosema: Ni sababu zipi zilizopelekea majina hayo kuibuka na kuwa majina ya mitaa? Kwa kutumia mbinu ya mahojiano na dodoso kutoka uwandani, mtafiti alikusanya data zinazohusiana na mada yake

ambazo ameziwasilisha na kuzichambua kwa kuzingatia lengo na swali la tatu kama anavyochambua katika maelezo yafuatayo.

### 4.5.1 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwamburi

Watafitiwa waliohojiwa kwenye mahojiano ya vikundi siku ya tarehe 24/8/2017 wameeleza kwamba, kwa kuwa mzee Mburi alikuwa maarufu katika maeneo mengi ya mitaa ya Pemba, hivyo basi watu kutoka maeneo mbali mbali waliokuwa wanaelekea kwa walisema kuwa tunakwenda kwa Mburi kutafuta matibabu. Jina la mtaa likageuzwa likawa Kwa Mburi badala jina la mtaa aliokuwa anaoishi mzee Mburi lililoitwa Mwisharifu. Kwa mantiki hiyo jina la mtaa la zamani likasahaulikana na jina jipya la Kwamburi likaibuka, lkashamiri na kustawi. Mtaa wa Kwamburi umekuwa ukiitwa kwa jinba hilo kuanzia uhai wa mzee huyo mashuhuri hadi leo ambapo tayari amseshafariki. Kwa hivyo jina la Kwamburi lilibuka kutokana na watu waliokuwa wakisema tunaenda kwa Mburi badala ya kusema tunaenda kwa Mwisharifu.

### 4.5.2 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Chanjamjawiri

Mtafiti alifanya majadiliano ya kina pamoja na kuchunguza majibu ya dodoso zake alizozigawa kwa watafitiwa wa eneo husika la Chanjamjawiri na mitaa ya jirani yake. Kwa kurejelea kipengele (4.3.2) mtafiti alibaini kuwa jina la mtaa wa Chanjamjawiri liliibuka kutokana na kuwa ni eneo ambalo alifia ama alikufa mtu aliyejulikana kwa jina la Mjawiri. Kijana huyu wa kiume alikufa katika eneo hilo kutokana na kuwa aliwakimbia Wareno waliovamia nyumbani kwao wakiwa na lengo la kumdhuru yeye na familia yake katika kipindi hicho cha ukoloni wa Kireno

(mwanzoni mwa karne ya 19). Watafitiwa wameeleza kuwa, Mjawiri ambae alikuwa mtoto wa Mkamandume alilazimika kuwakimbia Wareno ili kujikinga na shari zao. Katika kukimbia kwake ilifika wakati akachoka na inasemekana akaomba kwa Mwenyezi Mungu amdidimize aridhini ili asije akadhuriwa na Wareno hao. Dua hio ilijibiwa na akadidimizwa katika eneo la uwanda au wengine waliita chanjaa. Hapo alipodidimizwa mwishowe pakaitwa kwa jina la Chanjamjawiri; yaani chanjaa la Mjawiri. Jina hili linaendelea kutumika hadi leo.



**Picha 4. 3: Inayoonesha Chanjaa la Mjawiri lilivyokuwa hapo awali kabla ya kuwa makaazi ya watu.**

### 4.5.3 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Mkamandume

Kwa rejelea uchambuzi wa (4.3.3) na (4.4.3), mtafiti baada ya kufanya utafiti wake wa kina kwa wakaazi na watafitiwa wa maeneo husika yakiwemo ya Pujini na vijiji

vya karibu ya Pujini ambavyo ni Chanjamjawiri, Limani, Mtimbu, Chambani na kadhalika vyote vikiwa katika wilaya ya Chake chake Pemba. Mtafiti amebaini kuwa sababu kubwa ya kuibuka kwa mtaa wa Mkamandume ni, kutokana na muhusika mwenyewe Mkamandume ambaye alikuwa ni mtawala mwenye asili ya Kiarabu katika eneo hilo.

Mkamandume alikuwa mtawala katili, asiye na huruma. Kama ilivyokwisha kufafanuliwa kwenye kipengele (4.4.3), bwana huyu alikuwa akiwabebesha wakaazi wa eneo hilo mawe na kuwataka wasote nayo. Vilevile alikuwa akiwataka wakaazi hao wavunje chikichi kwa kutumia meno yao na alikuwa pia akiwahasi wanaume. Kwa kuwa tabia za Mkamandume zilikuwa ni mbaya na hazikubaliki katika jamii yeyote, wakaazi wa eneo hilo la Pujini na vijiji vya jirani wakaamua kupaita mahali hapo mtaa wa Mkamandume. Walipaita kwa jina hilo kwa lengo la kuendelea kukumbuka mateso waliokumbana nayo wakati wa uhai wa bwana huyo. Jina la mtaa wa Mkamandume hadi leo ni maarufu na linaendelea kutumika ipasavyo. Eneo la Mkamandume kwa sasa linatumika kama eneo la utalii na magofu ya kumbukumbu za makaazi yake hadi leo yanapatikana.

### 4.5.4 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwakitungu

Uchambuzi kuhusu jina na dhima/kazi ya kuibuka kwa mtaa wa Kwakitungu umefanyikakatika (4.3.4) na (4.4.4). Kama ilivyokwisha kuchambuliwa hapo nyuma kuwa Kwakitungu ni mtaa ambao unapatikana katika maeneno ya Gombani wilaya ya Chakechake Pemba. Sababu kubwa ya mtaa huo kuitwa kwa jina la mtaa wa Kwakitungu ni mtu anayeitwa Kitungu. Watafitiwa wameeleza kuwa Bwana Kitungu

alikuwa mpiga ramli mkubwa (mganga wa kienyeji) Kwa kuwa alikuwa akiagua katika ramli zake na kutoa majibu yenye kuwafaa vizuri wagonjwa wake mbalimbali. Utabiri wake huu ulifanya watu wa sehemu mbalimbali kumuamini na kupelekea kumbandika jina la Kitungu wakiwa na maana ya mtungaji au muaguji (mwenye kuagua). Jina hilo limempelekea kuwa maarufu hadi kusababisha mtaa huo kuitwa kwa jina lake la Kwakitungu ambalo hadi sasa linatumika na watu mbalimbali.

### 4.5.5 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Mwanamwari

Mtafiti kwa kuzingatia (4.3.5) na (4.4.5) amebaini kuwa Jina la mtaa wa “Mwanamwari” liliibuka kutokana na tukio la mwanamke ambae alikufa kwa kifo cha kuwashangaza watu waliowengi walioishi katika mtaa wa Mkumbuu ambako ndiko unakopatikana mtaa mdogo wa Mwanamwari. Inasemekana Mwanamwari alikufa kwa kuzama katika ardhi. Wazazi wa mtoto huyo wakaamua kujenga kaburi kwenye eneo alilozama mtoto wao. Tukio hilo lilisababisha mtaa huo kubadilishwa jina lake la asili (Kambalu) na kuitwa kwa Mwanamwari. Mtafiti alipofanya majadiliano na watafitiwa kutaka kujua sababu zaidi ya kuzama kwa Mwanamwari walidai kuwa, Mwanamwari alitokana na Afande Mwene na Ali Mwene. Wazazi hao walioa na mmoja wa mtoto wao wa kike akiwa bado mwari (hajaolewa) alipata ujauzito akiwa nje ya ndoa. Jambo hilo katika jamii ya Wapemba kwa wakati huo lilikuwa ni la aibu kubwa sana. Ili kuepuka aibu kwake na kwa familia yake Mwanamwari aliomba adidimizwe kwenye ardhi ili aepukane na aibu hiyo. Kwa bahati hayo yalitokea na dua lake likakubaliwa na kufanikiwa. Wazazi na walezi wa mtoto huyo waliamua kujenga kaburi katika eneo alilodidimia kwa lengo la kuweka kumbukumbu. Kwa kuwa jambo hilo lilikuwa si la kawaida eneo hilo lilibadilishwa

jina kutoka mtaa wa Kambalu na kuitwa kwa Mwanamwari. Watu wa kijijini hapo walipohama wakapaita Mkumbuu ingawaje sehemu alipodidimia Mwanamwari hadi leo panaitwa kwa jina la Kwamwanamwari.



**Picha 4. 4 Kaburi la binti aliyeitwa Mwanamwari**

### 4.5.6 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwabomba

Uchambuzi kuhusu mtaa wa Kwabomba ulitangulia kuelezwa kwenye (4.3.6) na (4.4.6).

Katika uchambuzi huo mtafiti alieleza kuhusu jina la mtaa wa Kwabomba (4.3.6) na kazi/dhima ya mtu anayeitwa Kwabomba (4.4.6). Mtafiti baada ya kufanya utafiti wa kina kwa wasailiwa/ watafitiwa, amebaini kuwa sababu ya mtaa wa Kwabomba

kuitwa kwa jina hilo ni kwamba jina hilo limetokana na mtu anayeitwa Bomba (jina la umaarufu) na jina lake halisi ni Omar Said Rashid. Bwana huyu aliitwa kwa jina la bwana Bomba kwa sababu alikuwa anapozungumza, huzungumza kwa sauti ya juu na kubwa kiasi ambacho hata kama mtu utakuwa mzito wa kusikia au yuko mbali yake anaweza kusikia vizuri pasi na kutumia kipaza sauti chochote. Bwana huyu kwa kuwa sauti yake ilikuwa kubwa na mwenye kupenda sana kuzungumza, sauti yake iliweza kusikika na hata kuwaudhi wengine. Kwa misingi hiyo watu hasa wanakijiji wakaamua kuuita mtaa huo Kwa bomba. jina ambalo hili hadi leo linaendelea kutumika na muhusika mwenyewe hadi mtafiti anaandika tasnifu hii, yupo duniani anaendelea na maisha.

### 4.5.7 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kisiwani Kwabintiabedi

Mtafiti amezingatia sana uchambuzi wa awali katika (4.3.7) na (4.4.7). Kwa ujumla sehemu hizi zilichambua kuhusu mtaa wa Kwabintiabedi. Kwa misingi hiyo, mtafiti amebaini kuwa ipo sababu iliyopelekea mtaa huo kuitwa kwa jina la Kwabintiabeidi. Binti Abedi ni jina la mwanamke wa Kiarabu aliyetoka Omani kuja Pemba kumfuata baba yake aliyeitwa Bwana Abedi bin Sleyumu. Sehemu aliyokuwa akiishi bwana Abeidi iliitwa kisiwani bondeni. Bwana huyu alikuwa ni mkulima. Mtoto wake Binti Abeidi alikuwa ni mchumi na mfanyabiashara aliyechangamka sana kuliko baba yake. Alipofika Pemba eneo hilo la Kisiwani, akamua kutumia fedha zake kununua mashamba mbalimbali hasa mashamba ya mikarafuu iliyo kwenye eneo hilo la Kisiwani. Jambo hili lilimpelekea kumiliki sehemu kubwa ya ardhi Kisiwani hapo. Kwa sababu ya kumiliki sehemu kubwa ya mashamba kisiwani hapo wanajamii wakaamua kupabadilisha jina na kupaita mtaa wa Kisiwani Kwa binti Abeid. Jina

hili limeendelea kuzoeleka hadi leo. Ingawaje baada ya kufariki Bwana Abeidi na mwanawe urithi wa mashamba hayo umemilikiwa na serekali ya mapinduzi ya Zanzibar.

### 4.5.8 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwakiburi

Mtaa wa Kwakiburi, uchambuzi wake umeanza kufanyika katika (4.3.8) na (4.4.8). Kwa mnasaba wa tangulizi hizo, mtaa wa Kwakiburi sababu kubwa ulitokana na mtu anayeitwa Bwana Ali Rasid Mussa. Bwaba huyu alikuwa ni tajiri mkubwa aliyeishi sana nchi za ulaya zikiwemo Uengereza na Kanada. Baada ya kuishi huko kwa muda mrefu bwana huyo aliamua kuhama na kuja kwao Pemba maeneo ya Bahanasa wilaya ya Wete. Bwana huyu aliweza kununua eneo kubwa la mashamba ya mikarafuu sehemu ya Bwagamoyo, wilaya ya Wete. Vilevile katika eneo hilohilo alijenga nyumba yake kubwa nzuri, skuli ya watoto wadogo (nursery), Kituo cha afya (dispensary) na bekari na sehemu nyengine aliwauzia watu na kuufanya mji uzidi kukuwa na kupenedeza hadi leo.

Mtafiti katika majadiliano yake na watafitiwa, alitaka kujua sababu ya jina kiburi ilikuwa ni nini? Maelezo kutoka kwa watafitiwa yalifafanua kuwa jina la mtaa wa Kwakiburi halitokani na sifa ya bwana Ali Rahid Mussa kwamba alikuwa na kiburi, la hasha. Pamoja na kuwa alikuwa tajiri lakini hakuwa na kiburi. Jina la kiburi lilitokana tangu bwana huyo alipokuwa mtoto mdogo alikuwa akipenda sana kutumia kibuli (kifaa kinachotumika kuhifadhia chai au hata kahawa). Kwa kuwa alipenda kutumia kifaa hicho ndipo babu yake akamwita kwa jina la “Kibuli” na baadae

“Kiburi” jina hili liliendelea kukuwa hadi kutumika kuwa ni jina la mtaa unaoitwa mtaa wa Kwakiburi ambapo bwana huyu ndie muasisi wa mtaa huu.

### 4.5.9 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Chambwaga

Data zilizokusanywa na mtafiti kuhusu mtaa wa Chambwaga zimeelezwa vyema (4.3.9) na (4.4.9). Mtaa huo unasababu zake timilifu za kuitwa kwa jina hilo. Bwana Haji Omar Faki ambapo umaarufu wake huitwa Chambwaga kama ilivyoelezwa alikuwa ni mtu mpenda utani kwa watu. Alikuwa ni mchezaji na mpiga ngoma, mvuvi na mfanyabiashara. Sababu ya kuibuka kwa jina hilo kumeelezwa l na mitazamo miwili tofauti ya watafitiwa. Mtazamo wa kwanza umedai kuwa jina Chambwaga limetokana na siku moja watoto wa ami zake bwana Haji walimuomba kaka yao awapigie ngoma nawao wacheze. Bwana huyo wakati anapiga ngoma hiyo watoto hao walianza kuimba:

“*cha...cha ... mbwaga, chambwaga dezo”*
*“cha...cha ... mbwaga, chambwaga dezo”*
*“cha...cha ... mbwaga, chambwaga dezo” x3*

Kuendelea kuimba kwa nyimbo hiyo kukamfanya bwana Haji kuacha kutumika jina lake halisi na kuitwa Chambwaga, jina ambalo lilizoeleka na kuwa maarufu hadi kupata fursa ya kuitwa jina la mtaa.

Mtazamo wa pili, alioubaini mtafiti ni kuwa sababu ya bwana Haji kuitwa kwa jina la Chambwaga inadaiwa ni tabia mbaya ya bwana huyo. Tabia yake kubwa mbaya ni israfu ikiwemo katika shughuli za harusi. Bwana Haji imedaiwa kuwa akialikwa katika shughuli za harusi hufanya israfu ya chakula hata kama hakimalizi hukiharibu

anaponasihiwa kuacha tabia hiyo hudai chambwaga dezo, yaani ni chakula cha dezo. Tabia hii ikamfanya azoeleke hadi kupelekea mtaa huo ulio karibu na maeneo ya Wingwi wilaya ya Micheweni kuitwa mtaa wa Kwachambwaga.

### 4.5.10 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwamchawi

Watafitiwa mbalimbali wameeleza kuhusiana na jina la mtaa wa Kwamchawi kama ilivyoelezwa katika (4.3.10) na (4.4.10). Katika ufafanuzi wa watafitiwa, mtafiti amebaini kuwa sababu kubwa ya mtaa huo kuitwa kwa jina la Kwamchawi lilitokana na bwana huyo aliyeitwa Bwana Omari Dadi Khamis. Watafitiwa wameeleza kuwa Bwana Omar alihamia mtaa wa Wingwi akitokea maeneo ya Kinazini wilaya ya Wete. Mara alipowasili hapo bwana Omar aliendelea na biashara zake za duka mtaani hapo. Watafitiwa wameeleza kuwa wakati akiwa mdogo, bwana Omari alijaaliwa bahati na kipaji kizuri. Bwana huyo alijaaliwa na Mwenyezi Mungu mara nyingi mambo mengi aliyokuwa akiyazungumza na kuyabahatisha hufanikiwa. Kwa tabia hizo, jina lake likaanza kubadilika na kuonekana kama mchawi kwa kuwa ni mbahatishaji mzuri. Kuendelea kutumika kwa jina hilo kukamfanya bwana Omari kuzoeleka hadi kupelekea jina hilo kuitwa kwa jina la mtaa wa Kwamchawi. Jina hili hadi sasa linaendelea kutumika.

### 4.5.11 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwasetimende

Kwa mujibu wa watafitiwa waliohojiwa tarehe 27-8-2017 Bwana Setimende alikuwa maarufu katika maeneo mbali mbali ya mji wa Wete. Hivyo watu kutoka maeneo walisema kuwa tunakwenda kwa Setimende kwa ajili ya kutengenezewa vyombo vyao vya usafiri badala ya kutaja jina la mtaa anaoishi Mzee Setimende lililojulikana

kwa jina la Mtemani. Watu hao waliweza kujisahaulisha jina la zamani la mtaa aliokuwa akiishi mzee huyo na kuita mtaa huo kwa jina jipya la Kwasetimende. Mtaa wa Kwasetimende umekuwa ukiitwa hivyo kuanzia uhai wake hadi hii leo ambapo mzee huyo ameshafariki.

### 4.5.12 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwakitazonge

Kwa kurejelea ( 4.3.12) na ( 4.4.12 ) mtafiti alibaini kuwa jina la mtaa wa Kwakitazonge liliibuka kutokana kuwa ni eneo ambalo aliishi mzee aliejulikana kwa jina la Kitazonge.

Hivyo basi watafitiwa walieleza kuwa Kitazonge alikuwa mtu ambae aliishi huko Makaani alilazimika kuishi katika mtaa huo kutokana na shughuli zake za kujitafutia riziki. Kitazonge alipenda sana kufanya hadaa kwa baadhi ya watu ambao aliwapa huduma katika kuwapatia tiba. Mtaa huo ulijulikana kwa jina la Kitazonge kuanzia uhai wake hadi leo ambapo mzee huyo ameshafariki.

### 4.5.13 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kiuyu Kwamanda

Kama tulivokwisha eleza katika ( 4.3.13) na ( 4.4.13 ) mtafiti baada ya kufanya utafiti wake kina kwa wakaazi watafiti wa maeneo husika yakiwemo Makangale na Kiuyu kwa Manda Wilaya ya Micheweni Pemba, mtafiti amebaini kuwa sababu kubwa ya kuibuka kwa mtaa wa Kiuyu KwaManda kumetokana na muhusika mwenyewe Mzee Manda ambae alikuwa maarufu katika eneo hilo la Kiuyu.

Mzee Manda alikuwa mtu mashuhuri mwenye asili ya Kimakonde ambae alihamia Kiuyu mnamo mwaka 1945, wakati huo msitu na kuanzisha makaazi yake hapo

alizidi kuwa maarufu kwa kuwa alioa na kupata watoto wengi watoto ambao waliongeza kuzidisha umaarufu wa baba yao. Hivyo Kiuyu kwaManda kulikuwa kukiitwa hivyo tokea uhai wake hadi leo hii mtaa huo unaendelea kuitwa Kiuyu Kwamanda.

### 4.5.14 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwashaamemata

Uchambuzi kuhusu ubainishaji wa majina ya watu mashuhuri pamoja na kazi zilizowapa umashuhuri watu hao katika kipengele ( 4.3.14 ) na ( 4.4.14 ) Kwashaame mata ni mtaa uliopo katika maeneo ya Micheweni wilaya ya Micheweni Pemba. Sababu kubwa ya mtaa huo kuitwa kwa jina la Kwashaame mata ulitokana na mtu aliejulikana kwa jina la Shaame ambae aliishi mtaani hapo.

Watafitiwa waliododoswa na kuhojiwa walikuwa na mtazamo miwili tofauti. Mtazamo wa kwanza ulidai kuwa Bwana Shaame akiwa mwanasiasa mashuuri ambapo mikutano yote ya kisiasa ilifanyika katika eneo la shamba yake.Hivyo kuendelea kufanyika kwa mikutano ya kisiasa katika eneo hilo kulimpelekea Bwana Shaame mtaa wake kuitwa kwa jina lake halisi yaani Shaame mata. Mtazamo wa pili umebaini kuwa alikuwa mvuvi maarufu kila alipoulizwa wakati akirudi pwani "Bashaame kumpata" yeye alijibu kuwa sepata ata ila hii myata. Myata ni chombo kilichotumika kunasia samaki. Kutokana na majibu hayo naye aliitwa Shaame mata kwa vile alikuwa maarufu sana na mtaaa anaoishi pia ukaitwa kwa jina la kwa Shaame mata hadi leo hii jina hilo linaendelea kutumika.

### 4.5.15 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwanondo

Watafitiwa mbali mbali waliohojiwa na kudodoswa tarehe 31-8-2017 wameeleza

kuhusiana na jina la mtaa wa Kwanondo kama ilivyoelezwa katika ( 4.3.15 ) na (4.4.15). Katika ufafanuzi wa watafitiwa, mtafiti alibaini kuwa sababu kubwa ya kuibuka kwa jina la Kwanondo lilitokana kwa kijana mwenyewe ambae alikuwa maarufu sana na alijulikana kwa jina la Nondo. Mtu huyu aliishi katika maeneo hayo ya kiuyu. Sababu ya shehe Juma kuitwa kwa jina la Nondo kwa mujibu wa watafitiwa linatokana na mtazamo miwili tofauti. Mtazamo wa kwanza unaeleza kuwa kijana huyo hapo awali alikuwa mvuvi wa kaa, na inaaminika kuwa yeye alivua kaa wengi kuliko wenziwe wote waliokuwa pamoja.

Kutokana na kuvua kaa wengi wavuvi wenzake walimtungia jina kwa kumuita Nondo, jina ambalo lilizoeleka na kuwa maarufu hadi kupata fursa ya kuitwa jina la mtaa. Mtazamo wa pili umebaini kuwa Bwana Nondo ambae ni mganga wa kienyeji aliefanya shughuli hizo za uganga karibu Afrika ya Mashariki kwa ujumla. Watafitiwa waliendelea kueleza kuwa katika ukoo wao kuna shetani aliejulikana kwa jina la Ngomanondo ambae ni shetani wao wa asili na anaetumiwa katika shughuli hizo za kiganga na yeye kijana huyo kwa wakati huu ndie aliefanya kazi hiyo.kutokana na sababu hii kijana huyo akaitwa kwa jina la Nondo. Kwa hivyo kwa kuwa Nondo ni maarufu sana jina hilo lilizoeleka na kuitwa jina la mtaa anaoishi hadi leo hii jina hilo linaendelea kutumika.

### 4.5.16 Sababu za Kuibuka kwa Mtaa wa Kwasururu

Habari zinazmuhusu bwana Sururu zimeanza kufafanuliwa kufafanuliwa kwenye (4.3.16) na (4.4.16). Mtafiti baada ya kufanya utafiti wake wa kina kwa wakaazi na wenyeji wa Sizini, alibaini kuwa, kuibuka kwa mtaa wa Kwasururu kumetokana na

muhusika mwenyewe mzee Salim Sururu ambae ni maarufu sana kuishi katika eneo hilo. Mzee Salim ambae ni mwenye asili ya kiarabu ana umashuhuri mkubwa sana. Bwana huyu alizaliwa Sizini na kulelewa Maskati Oman na alirejea Pemba (Sizini) akiwa tayari ameshaowa wake wawili. Kwa kuwa alikuwa tajiri wa pekee katika eneo hilo bwana huyu alianza kupata umaarufu hasa kwavile alikuwa akipenda kusaida watu wa aina mbalimbali na wenye hali tofauti za kimaisha. Hivyo kuwepo na kuishi mtaa huo kulisababisha mtaa huo kuitwa kwa jina la mtu huyo ambae ni mashuhuri. Hadi leo hii mtaa huo unaendelea kuitwa kwa jina la bwana huyo.

### 4.5.17 Sababu za Kuibuka kwa Mtaa wa Kwale

Uchambuzi kuhusu ubainishaji wa majina ya watu mashuhuri pamoja na kazi zilizowapa umashuhuri watu hao zimekwishaelezwa kwenye kipengele (4.3.17) na (4.3.18). Kwale ni jina la mtu aliyejulikana kwa jina la Mkwale aliyeishi katika maeneo ya Micheweni. Asili ya mtaa huo kuitwa kwa jina la mtu huyo inatokana na mzee huyo ambae alihamia hapo akitokea maeneo ya Tanga. Alikuja Micheweni kwa ajili ya kujitafutia maisha. Kwa mujibu wa watafitiwa waliohojiwa na kudodoswa tarehe 31/8/2017 mzee Mkwale alipohamia katika eneo hilo palikuwa msitu na hakuna mtu yeyote aliyekuwa akiishi katika eneo hilo Bwana Mkwale alivunja msitu na kuweka makaazi yake hapo. Hivyo watu wengine waliojenga baada yake walipaita Kwale kwa kuwa tayari walimkuta mzee Mkwale akiwa ameshahamia hapo. Hivyo kwa kuwa mzee Mkwale alikuwa maarufu sana jina la Kwale lilizoeleka na kutumika kuanzia wakati huo hadi leo hii jina hilo linaendelea kutumika ingawa mzee Mkwale amekwishafariki.

#### 4.5.18 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Kwamatunge

Watafitiwa mbalimbali waliohojiwa tarehe 01/9/2017 walieleza kuwa, sababu ya mtaa huo kuitwa kwa jina la bibi huyo (Bi Khadija) inatokana kuwa ni eneo analolitumia kuendeshea kazi yake ya kutoa tiba kwa wanajamii. Watafitiwa walieleza kuwa, bi Khadija ni bibi anaejishughulisha na kazi ya kutibu watu kutoka maeneo mbali mbali ya kisiwa cha Pemba. Bi Khadija ni mtabibu anaetibu maradhi mbali mbali yanayowakabili watoto na watu wazima. Anatibu watu wa jinsia zote wanaume na wanawakeWatafitiwa hao walieleza kuwa bibi huyo hutibu watu kwa kutumia dawa za asili (miti shamba) Kwahivyo mtaa huo umekuwa maarufu sana na kupelekea kuitwa kwa jina la mtu huyo aliye maarufu hadi leo hii.

#### 4.5.19 Sababu za Kuibuka kwa Mtaa wa Ngwachani

Kwa kurejelea uchambuzi katika kipengele cha (4.3.19) na (4.4.19) mtafiti baada ya kufanya utafiti wa kina kwa wakaazi na wenyeji wa mtaa wa Ngwachani, alibaini kuwa sababu kubwa ya kuibuka kwa mtaa wa Ngwachani ni muhusika mwenyewe ambae alikuwa kiongozi wa jadi katika eneo hilo na alikuwa akiishi katika mtaa huo. Diwani Ngwachani ambae alikuwa mtawala wa mwisho wa jadi kutoka Pemba na asili yake ni kutoka Pashia aliipenda sana jamii yake. Kiongozi huyu wa jadi alikuwa shupavu sana, kwani mara moja alikwenda Oman kuwaomba Waarabu waje wamsaidie kuwaondoa Mazrui walioitawala Pemba. Pia Diwani Ngwachani alikuwa na huruma sana na watu wake aliowaongoza na alipenda maendeleo katika jamii yake na jamii za wenzake. Watafitiwa walizidi kueleza kuwa Ngwachani hakuwa Mpemba halisi lakini alikuwa kiongozi mzuri kwa kuwa watu wake walimpenda na mtaa wao wakauita kwa jina la kiongozi wao (Ngwachani). Hivyo mtaa huo

umekuwa maarufu sana hadi leo hii. Mtaa huo umekuwa ukijulikana kwa jina la kiongozi huyo tokea uhai wake hadi hii leo ambapo amekwisha fariki miaka mingi iliyopita.



**Picha 4. 5: Makaazi ya asili ya Diwani Ngwachani**

Chanzo: Picha kutoka kituo cha makumbusho na utamaduni Pemba

**4.5.20 Sababu ya kuibuka kwa Mtaa wa Fiedel Castro**

Uchambuzi kuhusu jina na dhima/kazi ya kuibuka kwa mtaa wa Fiedel Castro umefanyika katika (4.3.20) na (4.4.20) kama ilivyokwishachambuliwa hapo nyuma. Fiedel Castro ilanza kuwa jina la shule na mtaa wote kuitwa kwa jina hilo. Sababu

kubwa ya shule pamoja na mtaa wote kuitwa kwa jina hilo la Fiedel Castro lilitokana na mtu ambae alikuwa Raisi wa Cuba aliyetoa msaada wa kuikarabati shule hiyo pamoja na kutoa samani mbalimbali zilizotumika katika shule hiyo. Msaada huo ulipelekea shule hiyo kubadishwa jina lake la asili na kuitwa jian la Raisi uhyo aitwae Fiedel Castro. Jina hilo lilipelekea kuwa maarufu na kusababisha mtaa mzima kuitwa kwa jina hilo ambalo hadi sasa linatumika kwa shule na mtaa wenyewe.

### 4.5.21 Sababu ya Kuibuka kwa Mtaa wa Ali Khamis

Mtafiti amezingatia kwa kina vipengele (4.3.21) na (4.4.21). Kwa hakika vipengele hivi vimechambua kwa kina kuhusu mtaa wa Ali Khamis Camp. kwa misingi hiyo mtafiti amebaini kuwa iko sababu iliyopelekea mtaa huo kuitwa kwa jina la Ali Khamis Camp.

Ali Khamis ni jina la mwanajeshi kutoka Tanzania Bara, aliyeletwa Pemba kwa lengo la kuendelea na kazi yake hiyo ya kulitumikia Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWT). Sehemu ambayo alikuwa akiishi iliitwa Vitongoji. Kutokana na umashuhuri wa mwanajeshi huyo kiutendaji na fani yake akiwa ndani na nje ya jeshi jina la kambi aliyokuwa akiifanyia kazi ikaitwa kwa jina la Ali Khamis Camp. Jambo hilo lilipelekea mtaa mzima kuitwa kwa jina hilo. Jina hilo linatumika hadi sasa na limepelekea kuibua majina mengine kama vile hospitali ya Ali Khamis Camp, shule ya Ali Khamis Camp pamoja na makanisa yaliyoko katika maeneo hayo yanaitwa kwa jina lake (Ali Khamisi Camp). Kwa ujumla kila kilichopo hapo kimenasibishwa na jina lake.

### 4.5.22 Sababu ya kuibuka Mtaa wa Pindua

Mtaa wa Pindua uchambuzi wake umeanza kufanyika katika (4.3.22) na (4.4.22) .Kwa mnasaba wa tangulizi hizo,mtaa wa Pindu sababu kubwa ni kuwaulitokana na mtu aliyeitwa kwa jina la Mohd Juma Pindua .Bwana huyu alikuwa mtu ambae ni mwanamapinduzi na alikuwa miongoni mwa watu kumi na mbili walioshiriki katika kupindua utawala wa kikoloni hapa Zanzibar na kuifanya Zanzibar kuwa huru.Bwana huyu alikuwa na uchungu na nchi yake,hivyo aliamua kujitolea muhanga kwa lolote ambalo limetokea katika nchi yake. Kitendo hicho cha ushujaa kilimpa umashuhuri mkubwa na kufanya mtaa huo kuitwa kwa jina lake Pindua.

## 4.6 Hitimisho

Sura hii imekuwa ni sura adhimu katika utafiti huu wenye mada: Kuchunguza majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitamtaa kisiwani Pemba. Kwa hakika sura hii imekuwa adhimu kwa sababu imefanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti ambayo ndio roho kuu ya utafiti huu. Kufanikisha majibu ya utafiti ndio kudhihirisha ukweli wa utafiti huo, sambamba na malengo ya utafiti. Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu pamoja na maswali matatu ya utafiti ambayo yaliwasilishwa na kuchambualiwa vyema kutokana na data za mtafiti alizozikusanya kutoka uwandani kama data za awali na zile data za nyongeza ambazo ndio data za upili za utafiti huu. Kwa udhati uchambuzi wa sura hii umekuwa na thamani kubwa katika utafiti huu kama ulivyotanguliwa na historia fupi ya kisiwa cha Pemba.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha muhtasari, matokeo na hitimisho la utafiti huu. Katika kazi hii mtafiti alichunguza majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa. Pia alitoa mapendekezo kutokana na jinsi alivyoona katika matokeo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Wakati utafiti huu ulipofanywa uliongozwa na malengo matatu. Lengo la kwanza ilikuwa ni: - kubainisha majina ya mitaa yanayotokana na majina ya watu mashuhuri kisiwani Pemba. Lengo la pili ni Kubainisha kazi au dhima maaalum zilizowapa umashuhuri watu teuliwa. Lengo la tatu ni kueleza sababu zilizopelekea majina hayo kuibuka na kuwa majina ya mitaa. Malengo haya yaliweza kupimwa kwa kutumia zana za utafiti na mbinu mbali mbali zilizotumika katika utafiti huu.

Ili kufikia malengo hayo mtafiti aliongozwa na maswali mbali mbali yaliyoenda sambamba na malengo mahususi. katika kujibu maswali hayo, mtafiti aligundua kuwa majina ya watu mashuhuri yana asili na sababu ya kuibuka kwake. Mtafiti alibainisha majina ya watu mashuhuri katika mitaa ya Pemba na kuyatolea dhima na sababu ya mitaa hiyo kuitwa kwa majina hayo. Pia majina hayo yalibainika kuwa

yametokana na mambo mbali mbali yanayojitokeza katika jamii husika. Aligundua kwamba watu mashuhuri waliowengi walikuwa na jina zaidi ya moja na majina yao ya utani ndiyo yaliyopata umaarufu zaidi. Majina hayo ndiyo baadae yaliyoibuka kuwa majina ya mitaa kutokana na kuhusiana kwake moja kwa moja na watu hao mashuhuri. Mitaa mingi ilipewa majina ya watu hao kwa sababu watu hao walifanya makaazi yao kwenye maeneo hayo. Wengine walifanya au walitokewa na matokeo yasiyokuwa ya kawaida katika maeneo hayo.

## 5.3 Hitimisho

Inaonekana kwamba kabla ya majina ya mitaa haijaibuka kutokana na watu mashuhuri husika walioelezwa kwenye utafiti huu kila mtaa ulikuwa na jina la awali. Kuja kwa watu hawa mitaa ikageuzwa majina na kutumia majina ya watu hawa mashuhuri. Kwa muktadha mtafiti anahitisha kwa kusema kuwa ni kweli kabisa kuwa watu mashuhuri wana umuhimu mkubwa kabisa katika kuibua majina ya mitaa kupitia majina yao.

## 5.4 Utoshelevu wa Nadharia iliyotumika

Kutokana na nadharia jumuishi ya Giles mtafiti aliweza kugundua kuwa majina ya watu mashuhuri yanatokana na majina ya viongozi, matukio ya kihistoria matukio ya kijamii pamoja na shughuli zinazofanywa na wanajamii. Hivyo mtafiti kwa kutumia nadharia hii aliweza kueleza kufafanua mambo mbali mbali katika jamii yanayolenga watu mashuhuri katika mitaa mingi hapa kisiwani Pemba jambo ambalo lilimsaidia mtafiti kuchambua kuwasilisha data zake. Pia nadharia ilisaidia katika kujibu maswali yaliyoongoza utafiti huu kwani imeonesha matumizi ya majina yalivyoweza

kuibua majina ya mitaa. Hivyo nadharia jumuishi ilikuwa muhimili wa kusimamia utoaji na upewaji wa majina ya watu na baadae kuwa majina ya mitaa.

## 5.5 Mapendekezo juu ya Tafiti zijazo

Wataalamu mbali mbali wameeleza kuhusu majina ya watu. Mtafiti amezungumzia juu ya majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Mtafiti amebaini kuwa kipengele cha majina ya watu mashuhuri kinahitaji kuangaliwa kwani imegundulika kuwa majina ya watu mashuhuri yanachangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba kama ambavyo mtafiti ameeleza. Hivyo imependekezwa kwa tafiti zijazo kujihusisha na athari za kutoweka kwa majina ya wanyama adimu wanaopatikana kisiwani Pemba. Pia ichunguzwe michango ya miti mikubwa katika kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba. Pia majina ya wanyama wakufugwa yanavyoibua majina ya mitaa ni vyema kuchunguzwa na kufanyiwa utafiti.

## MAREJELEO

Adam, J. & Kamuzora, F., (2008). Research Methods for Buisiness and Social Studies. Mzumbe Book Project. Morogoro, Tanzania.

Ally, J. & Mustafa, B. (1930). *Nahau –Al –Waadhih*. Beirut: Dar al-Kutub al-Ilmiyah.

Al-Zumor, A. Q. G., (2009). *A Social-Cultural and Linguistic Analysis of Yemeni Arabic Personal Names,* Abha: King Khaled University.

Backhaus, P. (2007). *Linguistic Landascapes: A Comparative Study, Urban multilingualism in Tokyo,* Great Britain: MPG Book Ltd.

Baitan, B. (2010). Morphosemantic Analysis of Ruhaya Person Names (Unpublished M.A Dessertation), University of Dar es Salaam, Tanzania.

BAKIZA, (2008). *Utamaduni wa Mzanzibar*. Zanzibar: BAKIZA.

Baver, H. D. R. (1979). *Chinese Family and Kinship,* Newyork: Colombia University Press.

Best, J. W. & Kahn, J. V., (1993). *Research in Education.* United State of America: Allyn and Bacon.

Boas, F., (1964). *"*On Geographical Names of the Kwakiuti Indians"Language in Culture and Society, A Reader in Linguistics and Anthropology. New York, Evaston and London, University of calfonia, Berkeley Harper and Row Publishers.

Buberwa, A. (2010). Investigating of Sociolinguistic Aspects of Place Names in Ruhaya in North-West Tanzania, Unpublished M. A Dissertation. University of Dar es Salaam, Tanzania.

Cameroon, K (1961). *English Place Names*. London: Exford University Press.

Chum, H. (1982*). Desturi na Mila Zetu*. Arusha: East Africa Publication Limited.

Chulk, O. O. (1992). *Names fromAfrica: Their Origin, Meaning and Pronoucition,* Chicago: John Publishing.

Edelman, L. (2010). *Linguistic Landscapes in the Nertherlands: A Study of Multilingualism in Amsterdam and Friesland.* Amsterdam: LOT.

Enon, D. C. (1998). *Educational Research, Statistics and Measurements.* Makerere University Press.

Khamis, A. M. & Madumula, J. S. (1989). *"Majina Yanayohusu Watu" Mulika* Na.21, Dar es Salaam: TUKI.

Kofi, A. (2006). The Sociolinguistic of Akan Personal name. *Nordric Journal of African Studies*, 15(2), 206-235.

Kombo, D. K & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Afrika.

Kofi, A (2006). *The Sociolinguistic of Akan Personal name. Nordric Journal of African Studies*, 15(2), 206-235.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology.Method and Techniques,* Second Revised Edition. New Delhi: New Age International (P) Ltd:

Massamba, D. P. B. (2004). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam. TUKI.

Manyasa, J. (2008*).* Investigating the Basis of Naming People in Kisukuma, Unpublished M.A. Dessertation. University of Dar es Salaam, Tanzania.

Mlacha, S. A. & Hurskainen, A. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*: Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y. P. & Wenzake (2009). *Isimu Jamii, Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Musere, J. (2000*). Traditional African Names*. Marryland: The Scarecrow Press Inc.

Mutembei, A. K. (2009). *UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Muzale, H. R. T., (1996*).* Linguistic and Social-Culture Aspects in Interlacanstrine Bantu Names." *Kiswahili* 61.28-49.

Omary, C. & Richerds, I. A. (1966). Person Names in Social-Cultural Context. *Journal of the Institute of Swahili Research*, 40(2). Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Redio Nour, (2013). *Kipindi cha Tutunze Historia Yetu, Oktoba, 18*. Zanzibar: Nour FM.

Saluhaya, M. C. (2010). *Kiswahili 1, Nadharia ya Lugha, Kidato cha Tano na Sita*. Dar es Salaam: Children Education Society(CHESO).

Schotsman, P. (2003). *A Grammar of Rumjambo Language of Tanzania (LOT) Project.* Dar es Salaam: LOT Publishers.

Seif, D. G. (2011). *Nyimbo za Jando katika Jamii ya Kikaguru, Kata ya Gairo,* Tasnifu M.A. Kiswahili.

Sengo, T. S. Y., (2009*). Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam. Al-amin Education and Research Academy.

Zawawi, Sh. M. (1998). *African Muslim Names: Images and Identities*, London: Africa World Press.

Zawawi, Sh. M. (1993). *What's in a Name? Unaitwaje? A Swahili Book of Names,* London: Africa World Press

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO Na.1

## MWONGOZO WA MASWALI YA HOJAJI KWA WAZEE NA VIONGOZI WA VIJIJI VYA PEMBA VILIVYOHUSISHWA NA UTAFITI HUU.

## MADA; KUCHUNGUZA MAJINA YA WATU MASHUHURI YALIVYOCHANGIA KUIBUA MAJINA YA MITAA KISIWANI PEMBA.

Mtafiti…………………………………Tarehe…………………………………

- Eleza jina kamili, umri ,jinsi, kijiji na mtaa unaoishi pamoja na shughuli unazojishughulisha nazo.
- Lengo la Utafiti huu ni kuchunguza majina ya watu mashuhuri yalivyochangia kuibua majina ya mitaa kisiwani Pemba.

  Tunaomba ushirikiano wako katika kutupatia taarifa sahihi juu ya hili.

1. Tutajie majina ya watu mashuhuri waliopo au waliokuwapo katika kijiji na mitaa tofauti unayoijua.

   ……………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………

2. Kuna vigezo gani vitumikavyo kutoa majina mbali mbali ya mitaa kisiwani Pemba?

   ……………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………

3. Unafikiri ni sababu zipi zilizopelekea majina ya watu hawa mashuhuri kupewa majina ya mitaa?

   ……………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………

4. Jee, ni shughuli gani zaidi walizokuwa wanajishughulisha nazo zaidi?

   ………………………………………………………………………………………

   …………………………………………………………………………………..…

   ….

5. Tutajie majina mengine matano ya mitaa ambayo asili yake yanatokana na watu mashuhuri.

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

6. Toa maoni yako kuhusu utoaji huu wa majina ya mitaa kwa kutumia umashuhuri wa mtu.

   ………………………………………………………………………………………

   ……..……………………………………………………………………………………

**AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**KIAMBATISHO Na.2**

**MASWALI YA MAHOJIANO KWA WATAFITIWA.**

Maelezo kuhusu mtafiti.

Ndugu mtafitiwa . Assalamu Alaykum warahmatullahi wabarakatuh.

Mimi ni mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Nafanya Utafiti kuhusu

majina ya watu mashuhuri yanavyochangia kuibua majina ya mitaa Kisiwani Pemba.Hivyo, naomba mashirikiano yako ili kufanikisha jambo hili.

Maelezo binafsi.

Jina kamili……………………………………………..(ikiwa utapenda)

Jinsi………………………………………..……………..

Umri (miaka)…………………………..…………………

Kazi………………………………………..……………..

Tarehe………………………………………………………………..

a) Unaishi mtaa gani?

b) Taja mitaa mengine mitatu inayoitwa kwa jina la watu maarufu.

i) ………………………………………………………………………

ii) ………………………………………………………………

iii) ………………………………………………………………………

3. Kwakawaida kila jina la mtaa lina chanzo au sababu ya kuitwa jina hil.Toa maelezo kuhusu mitaa minne unayoijua.

   i) Mtaa…………………………………………………………..

   ii) Sababu ya kuitwa jina hilo ……………………………………………

   iii) Jina kamili la mtu huyo ni lipi?...............................................................

iv) Mtu huyo alikuwa/anafanya kazi gani?

..............................................................................................................

4. Majina haya yana umuhimu gani kwa wanajamii?...........................................

5. Majina ya mitaa yana miundo tofautiya lugha ,kamavile majina ya wanyama, watu, miambatano ya majina nakadhalika .

a) Orodhesha majina matatu ya mitaa yenye majina ya wanyama na ueleze kwanini yakaitwa hivyo

i) …………………………………………………………………………

ii) …………………………………………………………………………

iii) …………………………………………………………………………

b) Taja majina mawili ya mitaa yenye mwambatano na ueleze kwa nini mtaa huo ukaitwa hivyo.

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

c) Taja majina matatu ya mitaa yenye majina ya watu na ueleze kwa nini yakaitwa hivyo.

i) …………………………………………………………………………

ii) …………………………………………………………………………

iii) …………………………………………………………………………

6. Majina hayo yanatambulisha nini katika jamii husika?

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

**AHSANTE SANA**

## KIAMBATISHO Na.3

MAJINA YA WATU MASHUHURI YALIYOCHANGIA KUIBUA MAJINA YA MITAA AMBAYO YAMECHUNGUZWA

Kwa mburi

Chanjamjawiri

Mkamandume

Kwa kitungu

Kwa mwanamwari

Kwabomba

Kwa bintiabedi

Kwa kiburi

Kwa chambwaga

Kwa mchawi

Kwa setimende

Kwa kitazonge

Kiuyu kwamanda

Kwa shaamemata

Kwa nondo

Kwa sururu

Kwale

Kwa matunge

Ngwachani

Fidel Castro

Ali Khamis Camp

Kwa pindua

KIAMBATANISHO Na. 4

PICHA YA FIDEL CASTRO

